

# *ONO LA PATIMO*

¶ ...Wakati Ndugu Neville alipokuwa akifanya matangazo hayo, ambayo Ndugu Moore alikuwa akisema hivi majuzi, akizungumza juu ya Roho wa Bwana, akaingia... akiingia jengoni. Alisema, "Kulikuwa kuzuri sana mle ndani hata nilifikiri Unyakuo ulikuwa umekuja mpaka nilipotazama kote, Nikaona hao wengine wameketi hapa," kasema, "la, haujaja bado, maana kama—kama wangali hapa basi ninajua ningali hapa." Kwa hiyo wakati mwingine Roho wa Bwana huwa mzuri hivyo kwetu.

<sup>2</sup> Tuna furaha sana kuwa na marafiki wengi ambao tunawaona humu jengoni. Wengi sana tusingejaribu kuwataja. Ndio kwanza nimwone, akiingia mlangoni, Ndugu Carpenter, yule mtu aliyeniuunganisha mimi pamoja na mke wangu katika ndoa. Ndugu Carpenter, amekuwa baraka kubwa kwetu hapa kanisani, na amekuwa baraka kwetu katika njia ya huduma, na huhubiri kokote, mahali popote. Nasi tuna furaha kuwa pamoja naye, loo, pamoja na wengine wengi sana.

<sup>3</sup> Sasa kuna swali lingine hapa ambalo nilipewa jana jioni:

**Ndugu Branham, je, wale wanawali watano wapumbavu wa Mathayo 25 wanahesabiwa kama masalia ya Mataifa? Nasikia ya kwamba hao wanawali watano wapumbavu waliokolewa bali inawabidi kuititia kwenye ule wakati wa dhiki kuu. Hii ni kweli? Kama ndivyo, hatima yao ya mwisho itakuwa nini? Je, wanaweza kuwa ni wale kondoo wanaotenganishwa na mbuzi katika Mathayo 25:33 na 34?**

<sup>4</sup> Mwanatheolojia hodari sana kulingana na yale mimi.... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...ninavyoliwazia pia, kwamba hao ni masalia, mwanamwali aliyelala ndiye masalia yaliyonenwa katika Ufunuo; wa uzao wa mwanamke unaoshika amri za Mungu na wana ushuhuda wa Yesu Kristo. Mwanamke atachukua ki—kipande cha kitambaa na kukitandaza chini; vema, sasa, hicho ndicho anachokatia ninii yake...ama anachukua bombwe lake na kuliweka popote apendapo, jinsi atakavyokikata hicho. Ndipo basi kile kilichosalia kinaitwa masalia, bali anachagua kukikatia mahali fulani kwa mawazo yake mwenyewe. Lakini kilichosalia kinaitwa masalia.

<sup>5</sup> Sasa, kama mtaangalia, kulikuwako na wanawali watano wapumbavu na watano wenye busara; wote walikuwa ni wanawali, waliotengenezwa kwa malighafi zile zile. Lakini, kwa uteuzi, Mungu alimchagua Bibi—arusi Wake kwa uteuzi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, akaweka majina yao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo aliyechinjwa kabla ya

kuwekwa misingi ya ulimwengu; kabla ulimwengu haujaanza, Mungu katika akili Yake, akiwa asiye na kikomo.

<sup>6</sup> Nasi tunalitumia neno hilo wakati mwengine, ni “kuchaguliwa tangu zamani,” lakini hakika linakwaza katika wakati huu wa kanisa tunaoishi. Hakika lilikuwa ni jambo kuu lililotumiwa katika siku za wafia imani, maana bila shaka waliliamini. Lakini wameliondokea sasa, wakaingia kwenye mawazo ya kisheria, fundisho la kisheria kanisani ambalo liliibuka . . . Ambalo lilikuwa ni jambo jema, kwa sababu wote walikuwa wameingia kwenye Ukalvini huko Uingereza hata hawakupata miamsho tena, naye John Wesley akajitokeza akihubiri fundisho la Kiarmenia ambalo liliusawazisha. Mungu daima atausawazisha.

<sup>7</sup> Kwa hiyo basi mwanamwali mpumbavu alikuwa ni wale wasiokuwa na mafuta kwenye taa zao, ambao ninaamini walitupwa kwenye giza la nje ambako kutakuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno. Basi kama mtalinganisha hilo, ama muhtasari wenu wa pambizoni, litarudi moja kwa moja tena kwenye ile dhiki kuu. Nami nafikiri hao ndio wanaobaki nyuma na kupitia kwenye ile dhiki kuu. Na ni somo zuri sana hapo, kama tungalikuwa na wakati wa kulingilia. Ikiwa wewe . . .

<sup>8</sup> Sasa, kumbukeni, nimesema hapo mwanzoni, ambapo unapoziskiliza kanda, “Mambo haya ni kulingana tu na vile ninavyoyaamini kwamba ni kweli.” Mnaona? Sasa, kama si sahihi, si—sijui kama si sahihi. Mimi . . . Nami ninaweza kusema tu yale ninayoamini. Wala sikusudii kuudhi hisia za mtu yejote. Hatuna budi kuyaweka tu kando tunapoingia, kisha tuchukue jambo lilosemwa, na kulichunguza, na tuone kama kweli ni Maandiko ama siyo. Hiyo ndiyo njia bora sana ya kulifanya. Halafu . . . Kwa sababu kwenye siku kama tunayoishi sasa, katika taifa ambalo limevunwa na kuvunwa tena na tena na tena na namna zote za kila kitu, vema, ni vigumu kuwafanya watu walishike kweli, kama ilivyo kwenye eneo lisilopata kuguswa. Ukiwaambia, wanaamini, hivyo ndivyo inavyotendeka.

<sup>9</sup> Lakini, sasa, mmoja atakuja na wazo *hili*, na mwengine atakuja na wazo *hili*, nasi tuna karibu makanisa mbalimbali mia tisa na kitu ya kimadhehebu, na kila moja linatofautiana (fundisho lake) na lingine; na inabidi kuwe na mtu aliyekosea, na mtu aliye sahihi. Kwa hiyo sasa thibitisho lake pekee ni, ni kulirudisha kwenye Biblia; mnaona, kuliachia Biblia. Sasa, mara nyangi, watu huweka tafsiri yao wenywewe. Bali tunajaribu kadiri tuwezavyo, kutowecka fasiri yoyote ya kibinadamu juu yake. Kuisoma tu jinsi ilivyo, na kusema, “Hivyo ndivyo ilivyo.”

<sup>10</sup> Halafu daima nimeona, kama utachukua tu yale Yeye aliyosema, itafanya kila kitu kiumane vizuri kabisa katika Maandiko. Ni kama tu kuweka mchezo fumbo pamoja, inakubidi kuangalia bombwe kabla ya kulitatua hilo fumbo vizuri.

Usipofanya hivyo, sikuzote nilisema, “Ungekuwa na ninii... Kwenye mandhari yako, ungekuwa na ng’ombe akila nyasi juu ya mti.” Kwa hiyo i—isingeonekana sawa.

<sup>11</sup> Na kama tu tukimwacha Roho Mtakatifu... Ni nani aliyeandika Biblia? Roho Mtakatifu aliwachochaea watu wakaiandika Biblia. Basi bila ya Roho Mtakatifu, haidhuru umeelimika vizuri kiasi gani, kamwe hutalielewa. Kwa maana hata Yesu alimshukuru Mungu ya kwamba alikuwa ameificha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na angeifunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza. Na kila mmoja wa wale wanafunzi alikuwa takriban hajasoma wala hana elimu ila mmoja, na huyo alikuwa ni Paulo. Naye Paulo alisema ilimbidi kusahau yote aliywahi kujuu kusudi ampare Kristo. Kwa hiyo aliliambia kanisa la Korintho, “hakuja na hekima ya wanadamu na hotuba kuu,” kwa sababu basi imani ya—yao ingekuwa katika hekima ya wanadamu, bali alikuja kwao katika nguvu na dhiihirisho la Roho Mtakatifu, kusudi imani yao ikae juu ya kazi za Roho Mtakatifu kulingana na Neno la Mungu. Na hapo ndipo tunapajaribu kushikilia kwa makini sana, sasa hivi, kwa sababu kabla juma halijaisha, ama wakati juma litakapoisha, mtaiona, hivyo ndivyo imekuwa hasa, uzi huo mdogo ukija kupitia kwenye wakati kote kote.

<sup>12</sup> Asanteni kwa kuuweka ubao juu zaidi kidogo. Huo unaonekana mzuri zaidi.

<sup>13</sup> Sasa, loo, sisi... Laiti tungaliendelea nalo msimu wote wa baridi kali, kusudi tuweze kukichukua tu Kitabu chote cha Ufunuo na kukipitia tu. Ni mafundisho mazuri sana humo ndani. Nami nakumbuka, nadhani imekuwa ni miaka ishirini iliyopita ama ishirini na mitano, wakati kanisa lilikuwa lingali jipy, tulianza moja... mapema kwenye msimu wa kupukutika, nalo likaendelea hata karibu msimu huo mwingine wa kupukutika majani, tukikipitia Kitabu cha Ufunuo.

<sup>14</sup> Sasa, ninakumbuka nikikichukua Kitabu cha Ayubu. Loo, Ndugu Wright! Nilidumu nacho muda mrefu sana hata hatimaye mwanamke mmoja akaniandikia na kuniuliza, akasema, “Ndugu Branham, hivi kamwe hutamwondo Ayubu kwenye lundo hilo la majivu?” Vema, nilikuwa nikijaribu kujenga hoja fulani, maana papo hapo ndipo kila kitu kilipolundikana, kufikia mahali hapo; kufikia mahali ambapo Roho wa Bwana alipomjilia, ndipo radi ilipoanza kumulika na ngurumo zikaanza kunguruma, Roho alikuja juu ya huyo nabii naye akakuona kule kuja kwa Bwana. Nami nilitaka kushindilia hilo, hiyo ndiyo sababu nilimshikilia kwenye lundo la majivu kwa muda mrefu, ili—ili tuweze kujenga hoja. Nami ninajua huenda likachosha, kidogo. Mimi hushikwa na wasiwas, pia, ninapomsikia mtu fulani akihangainakia kitu fulani, inaonekana kana kwamba angeendelea na kukifikia. Lakini labda Mungu anamwongoza mtu huyo kwa kusudi kwa ajili ya hilo.

<sup>15</sup> Sasa turejee kwenye masalia haya, kabla hatujaliondokea swalii hili. Natumaini nitalipata dhahiri. Hili...Hakika ninaamini ya kwamba masalia yamechaguliwa na Mungu. Ni—ninaamini, ya kwamba Mungu aliwachagua hao masalia kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; na amefanya hivyo kwa “kujuu Kwake tangu zamani.” Si neno...Sasa angalia huko *kuchagua tangu zamani*, unaona, maana ni neno dogo linalochoma mionganii mwa watu. Mnaona? Lakini Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, katika nia Yake kuu isiyo na kikomo, alilichagua Kanisa, akamchagua Yesu, akalichagua Kanisa, na angeweza kubashiri hapo mwanzo jinsi itakavyokuwa kwenye mwisho. Yeye...Kama Yeye hana kikomo, hakuna kitu asichokijua. Alijua kila kiroboto atakayekuwa duniani, na ni mara ngapi angepepesa macho yake. Sasa, hivyo ndivyo tu...na angetoa kiasi gani cha shahamu, na hao wote wangetoa kiasi gani kwa jumla. Hiyo haina kikomo, ni kutokuwa na kikomo; wewe—wewe...hakuna njia ya kulielezea. Naye Mungu, hivyo ndivyo alivyo, Mungu asiye na kikomo.

<sup>16</sup> Kwa hiyo, kama ukiangalia, Biblia ilisema ya kwamba katika siku za mwisho kwamba mpinga Kristo atakayekuwa juu ya nchi...

<sup>17</sup> Sasa sikilizeni kwa makini! Hilo ndilo dosari la pekee... Nadhani angeweza kupata mamilioni kwangu. Lakini juu ya Ndugu yetu wa thamani Billy Graham, hivi majuzi, yale mahubiri mazuri aliyohubiri Jumapili iliyopita, na hakika niliwazia ulikuwa ni ujumbe uliokuja kwa wakati mzuri. Na... lakini alisema ya kwamba “Shetani hata anawapoteza walio Wateule.”

<sup>18</sup> La, Biblia ilisema, “Angewapoteza walio Wateule *kama yamkini*.” Lakini haiwezekani, kwa sababu Mungu aliwachagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaona? Mwana-Kondoo...Yesu Kristo alikuwa ndiye Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Wakati Mungu hata anapoamua, anaponena Neno hilo, kamwe haliwezi kubadilika, kamwe haliwezi kugeuzwa. Mnaona, kwa sababu Yeye—Yeye hana kikomo, na Maneno Yake yatatimia.

<sup>19</sup> Wazieni tu, ninii yenywewe...dunia tunayokalia usiku wa leo ni Neno la Mungu liliodhihirishwa. Ulimwengu uliumbwa kwa vitu ambavyo hata havionekani. Yeye alisema tu, “Iwe,” na ikawa. Ni rahisi jinsi gani kwa Mungu huyo kuuponya mwili mgonjwa basi, kama Yeye anaweza kuumba kiumbe kwa kukineni tu. Mnaona, Neno Lake. Laiti tungaliweza tu kupata imani kuona kile Neno Lake lilicho! Tumefungwa sana na dunia na kuchanganyikiwa sana niani mwetu hata sisi...Loo, sijui mimi. Tumeshindilia mambo mengi sana, kombora kutoka kwa huyu, na kombora kutoka kwa yule, na—na imetufikisha tu mahali tumechanganyikiwa tu kabisa. Lakini kama ungaliweza

kukiondolea mbali kitu hicho chote, urudi ujue kwamba Yeye ni Mungu, na Maneno Yake hayawezu kushindwa kama vile Yeye asivyoweza kushindwa. Ndipo kama Neno hilo likishindwa, basi Mungu ameshindwa; na kama Mungu akishindwa kuna... Yeye si Mungu. Mnaona? Kwa hiyo... Nanyi kumbukeni, Yeye hawezi kusema jambo moja *hapa* na jambo lingine *hapa*; hana budi kudumu na uamuzi Wake wa kwanza kusudi apate kuwa ni Mungu. Kwa hiyo, tunaninii tu...

<sup>20</sup> Naye ametuomba tu jambo moja, kuamini ya kwamba yale aliyosema ni Kweli, Naye atayatimiza. Loo, ni zuri jinsi gani! Uilitarajia jambo la moja kwa moja litukie; wakati mwingine linahitaji tu imani kidogo. Halitafanya muujiza, bali kama ortalishikilia, litakutoa nje; dumu tu pamoja nalo. Kama Yeye alivyosema, "Mbegu ya haradali, ndiyo iliyo ndogo kuliko mbegu zote." Lakini hivi mlipata kuona, haradali haitachanganyikana na kitu chochote. Huwezi kuzalisha haradali na chochote, haitachanganyana. Na ikiwa una imani, imani kidogo tu ambayo haitachanganyikana na kutokuamini kwokwote ama ukanisa wowote ama mafundisho ya sharti, dumu tu pamoja na Mungu, dumu tu moja kwa moja Nayo, itakupitisha moja kwa moja kwenye ukungu, ikutoe nje kabisa. Naam! Dumu tu na imani hiyo.

<sup>21</sup> Sasa, hapo mwanzo, wakati Mungu... Biblia ilisema, katika Ufunuo, ya kwamba "Mpinga Kristo, katika siku za mwisho..." Sasa yaangalie makanisa haya yote yakiungana. "Mpinga Kristo, katika siku za mwisho, angewadanganya wote waliokuwa duniani ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Jina lako liliandikwa lini katika Kitabu cha Uzima? Kabla hatujakuwa na ulimwengu, ulichaguliwa kumpokea Roho Mtakatifu katika wakati huu.

<sup>22</sup> Nimejiunga na Eddie Perronet:

Nimetia nanga nafsi yangu katika ulimwengu  
wa raha,  
Nisisafiri bahari zenye dhoruba tena;  
Tufani huenda ikavuma kwenye kilindi kikali,  
cha dhoruba,  
Lakini katika Yesu tuko salama daima.

<sup>23</sup> Hakuna kitu kinachoweza kututenganisha (Mungu hawezi... halighairi Neno Lake. Na kama Yeye hana kikomo, na anakupa Roho Mtakatifu *hapa*, akijua ya kwamba atakupoteza *hapa* chini, Yeye anaendesha shughuli ya aina gani?), kama hujadanganyika katika uujuzi wako, kama una Roho Mtakatifu. Lakini angalia yale Biblia iliyosema, Waefeso 4:30, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata..." Uamsho unaofuata? Hilo linasikika

sawa? "Mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu!" Muda gani? Mpaka kwenye ukombozi wenu.

<sup>24</sup> Ukichukua behewa, ulipakie kwenye reli, basi wakati limepakiwa kikamilifu... Sasa, bado hawawezi kulifunga behewa hilo, inabidi mkaguzi apitie hapo. Naye analikagua, aone kama kuna kilicholegea kitakachotikisika. Huenda hilo behewa likaninii... Huenda behewa hilo limejaa kabisa, lakini kama lina mahali palegevu ndani yake, inakupasa kulipakia tena. Basi shida ndiyo hiyo, wengi wetu hatumpokei Roho Mtakatifu; wakati mkaguzi anapopitia hapo, anakuta mahali pengi palegevu, mnaona, kwa hiyo hatalitia muhuri bado.

<sup>25</sup> Mwanatheolojia mashuhuri alinijia hivi majuzi, ama si hivi majuzi, imekuwa ni miaka mitatu ama minne iliyopita, naye akasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ana haki."

Nikasema, "Hiyo ni kweli, sawa."

Kasema, "Mtu huyo angefanya nini zaidi ila kuamini?"

Nikasema, "Hayo ndiyo tu aliyoweza kufanya."

<sup>26</sup> Akasema, "Basi unaelekea wapi na upuuzi huu wa Roho Mtakatifu nje ya hiyo?" Sasa, mnajua ye ye aliкуwa ni Mbaptisti. Naye akasema—akasema, "Unaelekea wapi na huyu Roho Mtakatifu?" Kasema, "Kama mtu akiamini! Mara unapoamini, umempokea Roho Mtakatifu."

Nikasema, "La, la. Sasa, u—unaleta utata katika Maandiko, Maandiko hayajipangi Yenye. Mnaona? Paulo aliwaaliza, 'Je, mmepokea Roho Mtakatifu *tangu mlipoamini?*'"

Naye akasema, "Vema..."

<sup>27</sup> Nikasema, "Ni kweli kwamba Ibrahimu baba wa imani alitoa... aliкуwa na ahadi ya Mungu na alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kuwa ana haki, bali alimpa muhuri wa tohara kama ishara ya kwamba Yeye aliкуwa ameipokea imani yake."

<sup>28</sup> Sasa, kama Yeye hajapata kukutia muhuri kwa Roho Mtakatifu bado, kamwe hajapokea imani yako ndani Yake bado, una mahali palegevu. Unaona? Huenda ukaamini, naam, bali kuna mahali pengi palegevu. Lakini unapopakia vizuri mahali hapo pote palipolegea, basi anakutia muhuri kwa Roho Mtakatifu hata siku ya ukombozi wako. Hilo ni thibitisho la Mungu kwamba ameipokea imani ambayo ulikiri Kwake.

<sup>29</sup> Ibrahimu alikiri imani, naye Mungu akasema, "Nitakupa ishara sasa ya kwamba... kwamba nimekupokea." Naye akampa ishara ya tohara.

<sup>30</sup> Sasa, unapompokea Kristo kama Mwokozi wako na kumwamini Yeye na kumwomba ayasafishe maisha yako, ndipo

basi anaporudi na Roho Mtakatifu na kukupa ishara ya Roho Mtakatifu, basi umetiwa muhuri hata ukombozi wako.

<sup>31</sup> Behewa hili hapa, kama limelegea... Likiisha kupakiwa vizuri nao wanafunga huo mlango na kulitia muhuri, nalo-nalo limetiwa muhuri hadi kikomo chake, mashirika ya reli yangekupa kifungo cha maisha kama ungeuvunja muhuri huo. Haiwezi kuvunjwa. Limetiwa muhuri hadi kikomo chake; sio kwa kila mtu kwenye reli kuweza kulifungua na kuangalia ndani yake, na klichunguza na kulikagua lote, na kutupa vitu vichache nje, akaviingiza vitu vingine ndani. La, la!

<sup>32</sup> Kanisa *hili* litasema, vema, fundisho hilo la sharti, “*Hili si zuri, lile si zuri.*” Mungu anapokupa Roho Mtakatifu, imekwisha! Unajua mahali unaposimama, unajua yaliyotukia, nawe umetiwa muhuri kote hata siku ya ukombozi wako, kikomo chako cha safari hii ya duniani. Loo, jamani! Hilo linapaswa kufanya mtu ye yeyote kuwa tu na imani na kumwamini Mungu, asimame tu katika nguvu za Roho Mtakatifu.

<sup>33</sup> Sasa, wanawali hawa ambao hawakumpokea Roho Mtakatifu, (Mnakumbuka?) kitu pekee walichopungukiwa nacho kilikuwa ni mafuta kwenye taa zao. Hiyo ni kweli? Biblia ilisema *mafuta huainisha* “Roho Mtakatifu,” hiyo ndiyo sababu tunawapaka wagonjwa mafuta, na kadhalika, kwa sababu ni mfano wa Roho Mtakatifu. Sasa, halafu kama-kama Roho Mtakatifu hakuwajilia, hawakuwa Naye. Halafu alipokuja, walisema... Sasa, kwa wale wanawali waliokuwa na mafuta, kasema...

<sup>34</sup> Mnaona, walikuwa wamerudi kwenye wakati wa kanisa; kulikuwako na baadhi yao mle ndani waliokuwa ni watu wazuri bali hawakuwa kwenye Nuru ya nyota, ninachomaanisha, huku utambi umetiwa ndani ya mafuta. Mnaona, nayo ilikuwa imezima. Ilikuwa imezimika, walikuwa wamejitenga. Paulo alisema, katika siku yake, “Walijitenga na sisi, kwa kutokuwa na imani.” Mnaona, na wakawaacha, “Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wa kwetu.” Sasa, ilianza huko nyuma katika ule wakati wa mwanzoni wa Efeso na kufikia kwenye wakati huu leo hii. Jambo lile lile, kila mmoja wa nyakati hizo, kile kilichowapata kilishikana na nyakati hizi hapa chini. Tutaingilia hilo kindani katika kitambo kidogo.

<sup>35</sup> Sasa, angalia kwamba mwanamwali huyu, hata hivyo, aliingia mahali palipokuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno.

<sup>36</sup> Hebu niseme jambo hili, rafiki yangu mpendwa wa thamani; maana kwa kawaida humu kanisani, nijapo hapa, mimi huja tu hapa na kufanya ibada ya uponyaji na kuwaombea wagonjwa, na huko nje kote nchini mahali fulani. Lakini huu ndio wakati, nimekuwa nikiwaambia kwa muda mrefu, muweke dhamira yenu mfukoni mwenu. Sasa tunataka—tunataka kuja na kuwa

waaminifu na wa kweli sisi kwa sisi, kwa sababu tuko kwenye siku ya mwisho. Naam!

<sup>37</sup> Sasa, hapo ndipo ninyi Wanazarayo wa thamani na Wapilgrim Holiness chini ya utakaso mliposhindwa. Mnaona? Sasa, hivi mljua Yuda Iskariote alifikia mahali papo hapo? Yuda alimwamini Bwana Yesu kama Mwokozi, akamkubali kama Mwokozi. Naye pia alitakaswa. Alitakaswa, katika Yohana 17:17, hapo Yesu aliposema, “Baba, watakase kwa ile Kweli, Neno Lako ni Kweli.” Na Yeye alikuwa Neno. Vema!

<sup>38</sup> Katika Mathayo 10, walipewa nguvu za kuwaponya wagonjwa, kuwafufua wafu, kuwatoa pepo. Nao wakaenda katika sehemu zote za—za nchi na kuwatoa pepo, kisha wakarudi wakishangilia na kupiga makelele na kumsifu Mungu. Ndipo Yesu akawaambia, “Msifurahi kwa sababu kwamba pepo wanawatii, bali furahini kwa sababu majina yenu yako kwenye Kitabu cha Uzima.” Hiyo ni kweli? Naye Yuda alikuwa pamoja nao, Yuda alikuwa pamoja nao, lakini hiyo ilikuwa ni mwaka mmoja na miezi sita kabla Yesu hajasulubiwa kamwe.

<sup>39</sup> Sasa, ndipo ilipofikia kwenye Pentekoste, Yuda apate kumpokea Roho Mtakatifu na kadhalika, alionyesha alichokuwa. A—alimkana Yesu, na akawa msaliti Kwake. Na hapo hasa ndipo roho hiyo ilipokuja; moja kwa moja kupitia Luther, Wesley, ikalileta kanisa hilo hadi kwenye utakaso kwa maisha safi (watu safi, wazuri, watakatifu, wema sana uliopata kukutana nao), lakini inapofikia kwenye...wanapoanza kunena kwa lugha na kumpokea Roho Mtakatifu, Nazarayo, Pilgrim Holiness, Methodisti Huru, basi wanasema, “Huyo ni ibilisi.” Na papo hapo ndipo mnapomkufuru Roho Mtakatifu na kujifungia nje milele; “Kwa kuwa mtu ye yeyote atakayenena neno dhidi ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali atakayesema neno dhidi ya Roho Mtakatifu hatasamehewa kamwe.”

<sup>40</sup> Kumbukeni, wanafunzi wote walinena kwa lugha. Yesu Kristo alikufa msalabani, akinena kwa lugha. Uh-hum. Kwa hiyo kama huwezi kuwashughulikia hapa, kupendana nao hapa, na kule je? Kwao... Kama hawa ni pepo, vivyo hivyo na wale. Kwa hiyo mnaona pale mahali ilipoonyesha rangi yake? Huyu hapa yule mwanamwali anakuja, safi kama hao wengine, maisha safi. Nitayachukua makanisa ya Kinazarayo ya mtindo wa kale, makanisa ya Pilgrim Holiness, ambayo kweli yaliamini katika utakaso, huwezi kuyaelekezea maisha yao kidole; safi wavezavyo kuwa. Ni jambo zuri kwamba sisi sote tuishi namna hiyo. Hiyo ni kweli, huna budi kuishi hivyo.

<sup>41</sup> Sasa, tunajua tuna wengi sana katika Pentekoste walio waigaji. Hiyo ni kweli. Lakini almuradi tu unaona dola bandia, unajua hiyo ilifanyizwa kutoka kwa iliyo nzuri, iliyo halisi. Hiyo ni kweli. Na kuna—kuna Roho Mtakatifu halisi, Yule halisi ambaye hunena kwa lugha na kuonyesha ishara na maajabu, na

imekuwa hivyo tangu Pentekoste na kuendelea. Kwa hiyo hatuna budi kuwa na waigaji. Hatuna budi kuwa na mwanamke mwovu ambaye si mzuri, kumfanya mwanamke aliye halisi anawiri. Hatuna budi kuwa na usiku, giza jeusi, kuonyesha nuru ya jua ni nzuri sana. Hiyo ni kweli. Nawe huna budi kuwa mgonjwa, upate kufurahia afya njema. Nayo ni kanuni ya mema na mabaya; na ni—na daima imekuwa hivyo, na daima itakuwa, mradi tu wakati ungalipo.

Sasa, kwa hiyo, hapo ndipo kanisa lilipojiinua juu.

<sup>42</sup> Sasa, hivi Yesu hakusema ya kwamba “Katika siku ya mwisho,” katika Mathayo 24, “kwamba roho hizo mbili zingefanana sana hata zingewapoteza walio Wateule kama yamkini”? Uh-hum. Bali ye ye aliyechaguliwa tangu kuwekwa misingi ya dunia yuna Uzima wa Milele. Uzima wa Milele, huwezi kuuondoa. Ni wa Milele kama alivyo Mungu, huwezi kukoma kuwepo kadiri Mungu asivyoweza kukoma kuwepo. Hiyo ni kweli. Kwa sababu wewe ni sehemu ya Mungu, wewe ni mwana na binti wa Mungu, maisha yako yamebadilishwa nawe ni sehemu ya Mungu, una Uzima wa Milele. Loo, ninampenda. Nawe je?

<sup>43</sup> Sasa, mtu fulani alikuwa amenipa muhtasari hapa, swalidogo tu. Hatutachukua muda mrefu sana sasa kulijibu. Pia kumbukeni, kila unapoliweka swalidogo hapa, nitajaribu niwezavyo kulifikia nikiweza. Lakini hili lilikuwa ni swalimuhimu:

**Mtu mmoja alitaka kujua kama ni vibaya kwa mwanamke kushuhudia, ama kuimba, ama kutoa jumbe katika lugha, kufasiri jumbe, ama kutabiri, kanisani.**

<sup>44</sup> La, si vibaya, ni...almuradi tu inakuja mahali hapo kwa utaratibu. Mnaona? Kanisa liko katika utaratibu, na ni wakati tu...Njia halisi, ya kweli kufanya hivyo ni kwa hao wanaonena kwa lugha na kadhalika, jumbe zao zinatolewa kabla ya ujumbe kutoka mimbarani, kamwe si kwenye wakati huo; maana Roho Mtakatifu anatenda kazi tu kutoka mahali pamoja kwa wakati mmoja, kama Paulo alivyosema pale. Lakini wanawake wamekirimiwa unabii, na kukirimiwa lugha na fasiri, na kila kitu ila kuwa wahubiri. Hawapaswi kuwa wahubiri. Wamekatazwa kuhubiri makanisani, hiyo ni kweli, kuchukua mahali hapo, au kuwa mwalimu wala chochote kile kanisani. Lakini kuhusu karama, mwanamke ana hizo zote, anaweza kupata moja ama yoyote ya hizo karama tisa za kiroho kulingana na Wakorintho wa Kwanza 12, wala hajafungwa kwamba ujumbe wake haupaswi kutolewa mahali pake. Mnaona, kila ujumbe hungojea wakati wake.

<sup>45</sup> Pakitokea mtu anayenena kwa lugha, wala hapana mwenye kufasiri, na atulie mpaka pawepo na mfasiri. Mnaona? Nazo jumbe hizi kwa kawaida zinatolewa kabla tu ya mkutano.

Ndipo nabii . . . ama mhubiri, ambaye ni nabii wa Agano Jipyä, mhubiri, anapojoitokeza, Mungu anaanza kutenda kazi kupitia yeye, mnaona. Ndipo akiisha kumaliza, basi jumbe zinaanza, mwingine; wakati huo, kabla yake tu. Daima liko katika utaratibu, sikuzote. Lakini mwanamke kweli ana haki.

<sup>46</sup> Jambo la pili, ningetaka tu, kuchukua muda mfupi nikijibu hili, nitasoma kichwa cha maneno:

TAFSIRI YA IMANI TATU ZA BIBLIA MOJA INAANZA. Washington, tarehe 15 Oktoba. Wanachuoni wa Katoliki, Protestant na Wayahudi wakifanya kazi kwa pamoja wameanza tafsiri mpya ya pamoja ya Maandiko ambayo huenda ikathibitika kuwa Biblia rasmi iliyongojewa kwa muda mrefu.

<sup>47</sup> Mambo mengine zaidi humu ndani ningetaka kuyasoma kidogo kabla ya kutoa matangazo yake. Kwa maneno mengine, mnaona kile hasa tunachozungumzia, yale hasa Maandiko yanayosema yatatukia katika siku hizi, ya kwamba vitu hivi vitaungana pamoja vipate kufanya sanamu ya mnyama. Kweli kabisa. Wamelijaribu, na wanalishughulikia, na sasa wana nafasi ilioy bora sana waliyopata kuwa nayo ya kuliwasilisha, maana liko moja kwa moja mikononi mwao. Na hiyo ndiyo sababu hasa ninazileta jumbe hizi za kinabii, kwa sababu nafikiri ni wakati wake.

<sup>48</sup> Na kama kuna mtu yejote ambaye angerudi kila usiku, tutajaribu kuanza mapema na kuwaachilia mtoke mapema. Na endapo sitalimaliza somo, basi nitatangaza kesho yake asubuhi. Kama hatutamaliza mandhari ya 19, kifungu cha 9 hadi cha 20 usiku wa leo, tutaanza asubuhi saa nne. Tutawajulisha wakati wa kufunga ibada, jinsi tutakavyoendelea.

<sup>49</sup> Na ndipo kesho usiku kwenye kanisa la Efeso, kuanzia, kuendelea kote siku saba usiku: Efeso, Wakati wa Kanisa la Efeso; na Smirna; na Pergamo; na Thiatira; na Sardi; na Filadelfia; na Laodikia, Jumapili ijayo.

<sup>50</sup> Huku nikijua lulu hizi kubwa zilizowekwa barabarani, ni vigumu sana kutoziokota kwa mikono yangu mpaka wakati huo. Kuziona tu huko chini, na kumhisi Roho akila katikati ya watu, inanifanya tu kutaka kuruka ndani upesi sana na—na kusema kitu juu ya hizo; lakinin ananibidi tu kujizuia na kuziweka kwenye wakati wao na kwenye majira yao. Kwa hiyo kama ukikosa kuja usiku, hakikisha utaipata kanda ama njia fulani utakayouputa, kwa sababu ninataka uenee kila mahali. Nami nimefanya jambo hili kwa sababu najisikia kuongozwa na Roho Mtakatifu kufanya hivyo; hiyo ndiyo sababu pekee ninafanya hivyo. Nami, kama sikufikiri lingelilisaidia kanisa . . . Na katika siku hii, kumbukeni, wakati unakuja hivi karibuni ambapo hatuwezi kufanya mikutano hii, nawe huna budi kufanya hivyo

sasa wakati tungali na wakati wa kuufanya. Mnaona, hatujui ni wakati gani watakapoukomesha huu, sasa.

<sup>51</sup> Na kwa hiyo kutakuwako na muungano mionganoni mwa makanisa nao wataungana pamoja, wafanye kichwa cha muungano wa kanisa, ambapo tayari mna jengo kubwa la U.N. na kila dhehebu liko ndani yake. Nawe itakulazimu kuwa mfua si wa baadhi ya madhehebu hayo ama ufukuzwe. Na huo ndio wakati ambapo itatubidi kuonyesha jinsi tulivyo na tuhakikishe tunajua, sio kudhania, bali kujua BWANA ASEMA HIVI mahali unaposimama. Maskini Kanisa hilo daima limekuwa katika uchache, ni kundi dogo sana ambalo...uzi mdogo, kama kamba nye—nyekundu inayopitia katika Biblia, bali daima ndilo Kanisa. Nasi tunataka kulikumbuka hilo.

<sup>52</sup> Sasa maoni kidogo tu kabla hatujasoma tena. Asubuhi ya leo tumechukua Uungu Mkuu wa Ufunuo wa Yesu Kristo, ambaye Mungu alimfunua kwetu asubuhi ya leo kama Uungu Mkuu: MIMI NIKO aliye Mkuu (sio mimi *nilikuwa* au *nitakuwa*), MIMI NIKO, sikuzote. Nasi tunaona katika mlango huu wa kwanza wa Ufunuo, wa Ufunuo...Ni ufunuo wa nini? Yesu Kristo. Kitu cha kwanza anachojifunua hapa jinsi alivyo ni kipi? Mungu wa Mbinguni. Sio mungu wa utatu, bali Mungu mmoja. Mungu mmoja, Naye hujifunua Mwenyewe hivyo mwanzoni mwa Ufunuo. Na kulizungumzia mara nne katika mlango wa kwanza ili kusiwepo na makosa. Jambo la kwanza unalopaswa kujua, ni kwamba: Yeye si nabii, Yeye si mu—mungu mdogo, Yeye si mungu wa pili, Yeye ni Mungu! Yeye ni Mungu. Na kwa hivyo basi Ufunuo ilitokea, na bado tunaendelea nao usiku wa leo moja kwa moja wakati tukiupata utu Wake wenye sehemu saba za uhai Wake.

<sup>53</sup> Na, loo, Mungu atusaidie tunapofundisha Maneno haya. Ni—ni—nimeyassoma kama kwa mtazamo wa kihistoria, lakini ngojeni mpaka nitakapofika mimbarani hapa nipate uvuvio. Kwa sababu najisikia kwamba tumeketi pamoja katika mahali pa mbinguni katika Kristo Yesu, na kwamba Roho yenu, sehemu yenu, ulimi wa Moto (Roho Mtakatifu) aliye juu Yako anakuja kwa mwingine, na mwingine kwa mwingine, anauwasha Mwili mkuu wa Mungu na kuuwasha moto, na hapo ndipo funuo...

<sup>54</sup> Sasa, jambo tunalolizingumzia, niliulizwa swalii hili, “Wanawake wanapaswa...na kadhalika?” Hilo hasa ndilo lilitoliingiza kanisa katika machafuko yake hapo mwanzo, walikuwa wametoa uchaji wote kutoka kwa wasikilizaji na kuuweka mimbarani. Lakini Mungu ni Mungu wa wasikilizaji. Yeye hutenda kazi katika kila mwanadamu, anaishi katika kila moyo anaoweza kuingia. Yeye huwachukua hao watu wenye vipaji na kutenda kazi kupitia wao. Sasa, kama ibilisi hawezi kuwapata kwa jambo moja, basi yeye huja huku na kufanya tu mkusanyiko wa bure na kuwafukuza watu. Kama vile Paulo alivyosema, “Mnapokutanika, kama nyote mkinena kwa

lugha, naye mtu asiyefunzwa aingie, si atasema, ‘Mna kichaa! Wajinga!’? Mtu fulani akinena kwa lugha, na *huyu* na *huyu* nje ya utaratibu, na kadhalika, hilo halitafaa kitu. Lakini,” akasema, “basi kama mtu akitabiri na kuzifunua siri za moyo, basi watasema, ‘Hakika Mungu yu pamoja nanyi.’” Lakini mmoja akinena kwa lugha kwa ufunuo na kutoa tafsiri yake, kitu fulani cha kulijenga kanisa, ndipo kanisa zima linajengwa nacho. Kitu fulani ambacho kitanena na Mungu akinena katika lugha ambazo hatujui kitu juu yake na atampa mmoja na kuifasiri kwa mwingine, na kusema jambo fulani litakalotukia tu jinsi liliivyosemwa, basi mna Roho wa Bwana mionganoni mwenu. Na, loo, hebu na tushindanie hilo, enyi marafiki; hebu—hebu tudumishe moto huo ukiwaka.

<sup>55</sup> Sasa, kabla tu hatujafungua ninii... kitabu hiki rasmi kikuu cha Maandiko, sijui kama ingekuwa ni kazi kubwa mno kama tungeweza tu kusimama na kubadilisha mkao wetu kwa dakika chache tunapoomba.

<sup>56</sup> Mwenyezi Mungu uliyemleta tena Bwana Yesu kutoka katika wafu na umemkabidhi kwetu (baada ya miaka elfu moja mia tisa) kama Mungu wa Mbinguni asiyekosea, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili na kwa Uwepo Wake pamoja nasi siku baada ya siku katika mwenendo wetu wa kila siku. Nasi tuna furaha sana kujua ya kwamba katika majira haya ya kuchanganyikiwa wakati ulimwengu haujui la kufanya, wanachimba mashimo ardhini, nao wanajijengea ngome kwa zege, lakini, Ee Mungu, hawawezi kujificha na ghadhabu ya Mungu. Kuna tiba mo—moja tu, Bwana, nasi tuna furaha sana kwamba tuliiikubali: “Nitakapoiona ile Damu nitapita juu yenu.” Loo, jinsi tulivyo na furaha usiku wa leo kwa ajili ya ulinzi huo unaotosheleza kwa yote wa Damu ya Mwana-Kondoo wa Mungu, Kuhani Mkuu, akisimama Utukufuni usiku wa leo akifanya maombezi juu ya maungamo yetu. Tuna shukrani sana kuwa pamoja Naye usiku wa leo, yule Mnjenaji mkuu, Roho Mtakatifu mkuu, mpaka mafuta mkuu, Mtoaji mkuu wa Uzima.

<sup>57</sup> Na sasa, Bwana Mungu, nimewaita watu hawa pamoja hapa chini ya paa hili usiku wa leo, nasi tumekusanyika hapa kama kanisa ama sehemu yake, tumekusanyika sio katika jina la maskani hii ama katika jina la mtu yejote yule, bali katika Jina la Yesu Kristo. Jalia Roho aliyeutawala mwili Wake na nia Yake, na kumwongoza, aingie ndani yetu usiku wa leo na kulifasiri Neno na kulihubiri Neno, na kulipa mioyo yetu iliyo na njaa tunapomnjojea. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa utukufu Wake. Amina. (Ketini.)

<sup>58</sup> Sasa kwenu mlion na Biblia zenu, fungueni mlango wa kwanza wa Ufunuo na kuanzia kifungu cha 9; penseli zenu na karatasi, nami nitajaribu kuwapa tarehe chache na kadhalika ninapoendelea.

<sup>59</sup> Sasa, hii kweli...Asubuhi ya leo ilikuwa zaidi sana ni namna ya mahubiri, tukiweka msingi juu ya Uungu, wa Ufunuo; Mungu akifunuliwa katika Kristo. Ni wangapi wanaoamini Hilo? Mungu alifunuliwa katika Kristo, Yehova akifunuliwa katika Kristo. Sasa Mungu atafunuliwa wapi? Katika Kanisa Lake, pamoja na watu Wake, ndani yetu. Roho yule yule, kazi zile zile, madhihirisho yale yale, upendo ule ule, msamaha ule ule, uvumilivu ule ule, wema, subira, amani, rehema, yote yaliyokuwa ndani ya Kristo yamo ndani ya Kanisa. Kumbukeni, kumbukeni hili: yote aliyokuwa Mungu aliyamimina ndani ya Kristo (Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili), na yote aliyokuwa Kristo aliyamimina ndani ya Kanisa. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Utatu wa Mungu, Mungu akidhihirishwa katika njia tatu mbalimbali: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

<sup>60</sup> Ufunuo ulionyesha ya kwamba Yeye si miungu watatu, wala hajakatakatwa katika vipande vitatu. Bali Yeye ni Mungu mmoja ambaye alikuwa Mungu katika siku za Ubaba, alikuwa Mungu katika siku za Uwana, Yeye ni Mungu katika siku za kipindi cha wakati wa Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule. Sio watatu mbalimbali, sio watu watatu, sio nafsi tatu. Yeye ni Mtu mmoja, nafsi moja. Huwezi kuwa nafsi bila kuwa mtu. Watu wengine walisema, "Yeye si watu watatu, bali Yeye ni nafsi tatu." Huwezi kumgawanya huyo; maana kama Yeye ni nafsi, Yeye ni mtu; hana budi kuwa mtu apate kuwa nafsi. Kwa hiyo Yeye ni Mtu mmoja, nafsi moja; yeye yule jana, leo, na hata milele; Alfa, Omega; Yeye aliyekuwako, aliyecko, na atakayekuja. Loo, Yeye ni YOTE tu. Ninapenda hilo.

<sup>61</sup> Angalia tabia Yake, maisha Yake, matendo Yake. Zinapaswa kudhihirishwa papa hapa maskanini, kama tu ilivyokuwa katika siku Zake. (Sisemi hii kwa chuki; Mungu anajua hilo.) Sio hapa tu, bali kote ulimwenguni. Nina furaha ya kwamba ndivyo ilivyo. Ndipo tunajua mahali tunaposimama kwa sababu tuna Roho yuyo huyo ndani yetu, akitenda kazi pamoja nasi na akionyesha ya kwamba Yeye yuko hapa. Sio sisi, ni Yeye; hatuwezi kufanya mambo hayo, ni Mungu. Isitoshe, katika ulimwengu wa kisayansi, Yeye aliruhusu picha Yake ipigwe. Pamoja nasi, ndani yetu, kutuzunguka, juu yetu, kupitia kwetu, akitenda kazi ndani na nje yetu. Loo, ni zuri jinsi gani!

<sup>62</sup> Walizoea kuimba wimbo mdogo:

MIMI NDIMI niliyesema na Musa, katika  
kichaka kilichowaka moto,  
MIMI NDIMI Mungu wa Ibrahimu, Nyota ya  
Asubuhi Inayong'aa.  
MIMI NDIMI Ua la Uwandani; loo, ati mlisema  
nilitoka wapi?  
Je, mnamjua Baba yangu, ama mwaweza kujua  
Jina Lake?

Loo, mwasema mimi kuwa ni nani, ama  
mlisema nilitoka wapi?  
Je, mnamjua Baba yangu, ama mwaweza kujua  
Jina Lake?  
MIMI NDIMI Alfa, Omega, mwanzo kutoka  
mwisho,  
MIMI NDIMI uumbaji wote, na Yesu ndilo  
Jina.

<sup>63</sup> Loo, ni ajabu vipi, huo Ufunuo! Sasa, kumbukeni, hamwezi kuupata kwa wanatheolojia, hauji jinsi hiyo. Utakuja tu kama ufunuo. Ubatizo wa maji, kwa kutumia Jina la Yesu Kristo, unaweza kutolewa tu kama ufunuo. Yesu na Mungu wakiwa Mtu yule yule unaweza tu kuja kama ufunuo. Biblia nzima imejengwa juu ya ufunuo. Kanisa zima limejengwa juu ya ufunuo. Mathayo 17 inasema, “Kwa kuwa nilisema, ‘Juu ya mwamba huu (ufunuo wa kiroho) nitalijenga Kanisa langu, na malango ya kuzimu hayawesi kulishinda.’” Tulimpa mtu ye yote changamoto atuonyeshe, mahali popote, historia ama Maandiko, ambapo palikuwapo na watu wowote waliobatizwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu” nje ya kanisa Katoliki mpaka kwenye siku ya Martin Luther. Ndipo kanisa la Kiprotestanti, lilikuwa . . .

<sup>64</sup> Na kila uovu . . . Sikilizeni, tunapoingia kwenye nyakati za kanisa. Kila uovu uliokuwa kwenye kanisa hilo la kwanza, ulipanda juu ya hilo lingine. Liliendelea tu kushuka mpaka hatimaye linaishia katika ukengeufu mtupu katika siku ya mwisho. Kila uovu unaendelea tu kupanda kwenye kila kanisa, kila itikadi ndogo ilioanza. Kama vile katika Mwanzo, ule mzabibu, ulianza kukua, ukajipenyeza kanisani na kutokeea katika siku za mwisho. Si ajabu Biblia ilisema, “Heri wale watakaoepuka kwenye siku hiyo.” Naam, bwana, watakaoyaepuka mambo haya yote.

<sup>65</sup> Sasa mwombe Mungu aninii . . . wakati tukizungumzia juu ya Ufunuo, mwombe akupe ufunuo wa Hili. Kwa kuwa linaweza tu kujulikana kwa ufunuo, nawe unaweza tu kuokolewa kwa ufunuo. Una ujuzi Wake, kielimu, bali huwezi kuokolewa mpaka lifunuliwe kwako. “Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu.” Hivyo ndivyo Biblia isemavyo. Hakuna mtu anayeweza kusema Yesu ni Kristo mpaka awe amempokea Roho Mtakatifu. Huenda akasema, “Mchungaji anasema hivyo, Biblia inasema hivyo.” Hizo ni kweli. “Kanisa linasema hivyo.” Hiyo ni kweli. Lakini wewe mwenyewe hujui mpaka Roho Mtakatifu amekufunulia *wewe*, Naye anakuwa ndani *yako*. “Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu.” Sio kwa maarifa, sio kwa akili.

<sup>66</sup> Watafanyaje Biblia ambayo . . . Kujaribu kuibana, kuifanya iwafae Wayahudi, Wakatoliki, na Waprotestanti, wakati wao wanatofautiana kama usiku na mchana. Nilidhani Wayahudi

wanajua vema kuliko hivyo; nafikiri labda wakati wake wa kuja umewadia, wakati lote halina budi kuingia katika ukengeufu huu mkuu. Kwa hiyo, na mambo yote kumbukeni tu, hatuwezi kulikomesha, bali jambo tu tunaloweza kufanya ni kuirusha Nuru huko nje, labda tujitoe mhanga kama wafia imani na kuondoka, kwa hiyo hivyo ndivyo tu tunavyoweza kufanya hilo. Lakini itawabidi wengi kufanya hivyo. Na kwa hiyo hivyo ndivyo Biblia ilivyopangwa na mambo ambayo tunayaingilia. Kama nisipoangalia, nitaliendea.

<sup>67</sup> Sasa, jambo la kwanza katika Kitabu cha Ufunuo, kinaanza kwamba ni Ufunuo wa Yesu Kristo, kwamba Yeye ni nani. Sasa, Yesu Kristo ni Mungu Mwenyezi. Tunajua hilo. Ni wangapi wanaamini hilo? semeni “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Yeye ni Mungu Mwenyezi, Naye ana Jina moja. Jina hilo ndilo jina pekee walilopewa chini ya Mbingu ambalo huna budi kuokolewa, Yesu Kristo. “Ni kwa nini wanaliogopa Hilo kwenye kidimbwi?” ndicho kitu nisichoweza kushangaa. Uh-huh. Mnaona? Ni kwa sababu kwamba ile roho ilinyemelea huko nyuma kabisa kwenye Wakati wa Smirna; na kujiingiza moja kwa moja kwenye wakati huo mkuu wa giza, na kulifanya fundisho, nayo ikaja moja kwa moja pamoja nalo katika siku hii ya mwisho. Sasa, angalieni tu historia na Biblia tunapopitia kwenye juma hili, jinsi—jinsi inavyovitoa vitu hivyo nje.

<sup>68</sup> Sasa jambo la pili. Ulitolewa na Kristo kwa Yohana, kwa mkono wa malaika, upewe (nini?) makanisa Yake, kulifunulia makanisa Yake. Nazo zile nyota saba mkononi Mwake zilikuwa ni wale wajumbe saba wa yale makanisa saba. Na kila mtu atakayepata kuwa na Ujumbe, ataupata, Ujumbe ule ule wa kweli ulioanza hapo mwanzo.

<sup>69</sup> Isitoshe, tutakapofikia kwenye mahali hapo penye kilindi pale, kuona jinsi ambavyo Mungu aliviingiza vitu hivi ndani, ni ajabu sana. Litawafanya tu mpaze sauti. Ningeninii, ningeyasoma, kisha nitembee-tembee huku na huku kidogo na kulia, nirudi na kuketi chini tena, kisha nitembee kidogo. Nina furaha sana nikijua hilo: Mungu aliturehemu hivi jinsi gani kuturuhusu kuona kitu hicho katika saa tunayoishi? Mbona, ni kama vile Yesu alivyosema, “Mtu mmoja aliuza yote aliyokuwa nayo apate kununua almasi fulani.” Unauuzia ulimwengu, mambo ya ulimwengu, na kila kitu kinachohusu kitu chochote kile, upate Hili. Hiyo ni kweli, tia nanga yako yote juu ya Hilo. Ndiyo nanga ya nafsi kuona ufunuo Wake wa Neno Lake.

<sup>70</sup> Sasa, yejote asomaye Hilo amebarikiwa. Hiyo ni kweli? Nasi tulisema asubuhi ya leo, kama huwezi kusoma, yejote atakayelisikia likisomwa, amebarikiwa. Sasa, linaanza na baraka hata kwa wale watakaoketi na kusikiliza likisomwa, na ni laana juu ya mtu yejote atakayejariku kuongeza lolote Kwake ama kuondoa lolote Kwake. Basi kama Biblia inafunua dhahiri kwamba Yesu alikuwa ni Mwenyezi Mungu, basi ole

wake yeye atakayeonda kutoka humo. Naam. Ni ufunuo. Kila atakayeongeza lolote . . . Ni kanuni nzima ya—ya Ufunuo; ndicho Kitabu cha mwisho cha Mungu, Maneno Yake ya mwisho, Yake ya mwi—. . . Na ufunuo wowote unaoenda kinyume na Huo, ni wa unabii wa uongo; sio Mungu, maana hii ndiyo Kweli.

<sup>71</sup> Basi, kumbukeni, hiki ndicho kitabu pekee katika Biblia ambacho Kristo alikiidhinisha, Mwenyewe. Wazia hilo! Kitabu pekee, ni ufunuo wake Mwenyewe. Kitabu pekee ambacho Yeye alitia muhuri Wake juu yake, na kuweka baraka Zake na laana Zake. Baraka kwa wale watakapokea, laana kwa wale ambao hawatakipokea.

<sup>72</sup> Sasa—sasa tuingie kwenye kisiwa cha Patimo sasa tupate kuanza, kifungu cha 9. Jambo la kwanza, tunataka kusema ni . . . Jina la huu ni: *Ono la Patimo*. Lilitukia katika A.D., kati ya A.D. 95 na 96. Mahali hapo palikuwa ni kwenye kisiwa cha Patimo. Mahali penyewe ni maili thelathini kutoka kwenye pwani ya Asia Minor, magharibi, kukingama kanisa la Efeso, katika Bahari ya Aegeani iliyopakana na ya Mediterania. Hapo ndipo kilipo.

<sup>73</sup> Wazieni! Sasa, kisiwa kidogo kilicho maili thelathini kutoka kwenye pwani ya Asia Minor, katika Bahari ya Aegeani. Kukingama tu kanisa la Filadel—. . . ama kanisa la Efeso, ambapo Ujumbe wa kwanza ulitolewa, ambapo Yohana alikuwa ndiye mchungaji wakati huo. Kwa maneno mengine, aliangalia moja kwa moja mashariki naye alikuwa akiangalia moja kwa moja kwenye kanisa lake, kutoka mahali alipokuwa. Nao Ujumbe wa kwanza ulikuwa ni kwa kanisa lake, ambalo liliwakilisha wakati wa kanisa. Vema, ono hilo alipewa Mtakatifu Yohana mtawa, aliyekuwa mchungaji wa kanisa la Efeso wakati huo.

<sup>74</sup> Hali ya kisiwa hiki ilikuwa ni namna gani? Kilikuwa wapi, na katika hali gani? Vema, kinajulikana katika historia kama kisiwa cha mawe kilichojaa nyoka, nge, mijusi, na kadhalika. Ni maili thelathini mzunguko, na kimejaa mawe. Kilitumiwa, katika siku za Yohana, kama Alkatrazi. Mahali ambapo himaya ya mfalme mkuu wa Kirumi iliwhamishia wahalifu, wahalifu wabaya sana, ambao wasingeweza kuwaweka gerezani na kadhalika, wangewaweka huko kwenye kisiwa hicho wapate kufa; wawaache wakae huko mpaka watakapokufa.

<sup>75</sup> Swali: Sababu ya Yohana kuwa kule? Mtauwa, mtu mwenye haki, mtu mwenye sifa nzuri, tabia nzuri, hajapata kuingia kwenye matatizo, kwa nini mtu huyu akawa kule? Biblia ilisema, “Kwa ajili ya Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo.”

<sup>76</sup> Sasa tumepata mandhari yake. Kisiwa cha Patimo, katika Bahari ya Aegeani, maili thelathini kutoka pwani, takriban maili thelathini mzunguko, mawe-mawe, kilichojaa mijusi na nge na kadhalika, na kilitumika kama jela (kama Alkatrazi ilivyo). Wanamchukua mfungwa wasiyeweza kumweka humu

gerezani, wanainii... mhalifu mbaya sana, wanamweka huko nje kwenye Alkatrazi.

<sup>77</sup> Na sasa walimchukua huyu Yohana mtakatifu mtauwa... mwanafunzi wa mwisho, na ambaye ndiye pekee aliyekufa kifo cha kawaida. Yohana, kabla ya kwenda kwenye kisiwa hiki, alishtakiwa kwamba ni "mchawi," naye akachemshwa kwenye pipa la grisi kwa saa ishirini na nne, bila kumwunguza. Huwezi kuchemsha Roho Mtakatifu amtoke mtu...?... Wakamchemsha kwa saa ishirini na nne kwenye pipa la mafuta, pasipo kudhurika. Ndipo wakasema, sababu iliyotolewa na Wa-Warumi, ni kwamba, "Yeye alikuwa ni mchawi, ndipo akailoga ile grisi." Yale nia ya kimwili inayoweza kuwazia! Sasa, mnaona, wanapotuita, "wasomaji wa mawazo, na wapiga ramli, na Beelizebuli," mnaona mahali roho hiyo ya kale ilikotoka? Lakini mnaona mahali Roho halisi anakotoka? Ni nyakati za kanisa. Mnaona? Saa ishirini na nne, akachemshwa katika grisi yenye joto iliyokuwa imechemka sana, na hata haikumgusa. Loo, jinsi Mungu alivyomjengea ngome ndani Yake kwa Roho Wake Mtakatifu. Kazi yake haikuwa imemalizika.

<sup>78</sup> Walimweka kwenye kisiwa hicho kwa muda wa miaka miwili. Basi wakati Mungu alipokuwa naye huko peke yake, aliandika Kitabu cha Ufunuo jinsi Malaika wa Bwana alivyomfunulia. Halafu basi mara hayo yalipokwisha, alirudi nchini mwake na kulichunga kanisa Efeso. Naye akafa na akazikwa Efeso, Yohana mtauwa.

<sup>79</sup> Loo, ni mandhari ya jinsi gani sasa! Vema, kanisa wakati huo likiwa chini ya Yohana ama chini ya mateso makuu, Yohana anaandika kifungu cha 9:

*Mimi Yohana, niliye ndugu yenu... katika mate-... na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso, na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kitiwacho Patimo, kwa ajili ya Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo.*

<sup>80</sup> Kwa maneno mengine, ye ye alilichukua Neno la Mungu na alikuwa akilithibitisha, kwamba lilikuwa ni Neno la Mungu, ndipo Kristo akarudi kupitia kwake na kushuhudia kwamba alikuwa sahihi. Haya basi. Neno la Mungu likidhihirishwa ndani yake, likithibitisha ya kwamba ye ye alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Basi wasingeweza kukana jambo Hilo, kwa hiyo iliwabidi kumwambia ya kwamba alikuwa ni "mchawi." "Aliiloga ile grisi nayo haingemdhu, kisha akawaloga watu wala hawakuponywa, naye alikuwa ni mpiga ramli ambaye asingeweza... Namna fulani ya mtu mbaya, pepo mba-... pepo mchafu." Na hiyo ndiyo sababu walimweka huko nje, walidhani alikuwa hatari kuwa mionganoni mwa umma. Lakini alikuwa tu akiyatekeleza mapenzi ya Mungu, naye Mungu alikuwa na kusudi fulani chini ya hali hiyo yote.

<sup>81</sup> Asingeweza kumtumia, na mateso yote na kadhalika, maana watakatifu walikuwa wakija, “Loo, Ndugu Yohana, tutafanya nini juu ya jambo *hili*? Na sisi tutafanya nini?”

<sup>82</sup> Yohana alikuwa nabii, tunajua hilo. Na kwa hiyo walikuwa wakiuliza maswali haya, kwa hiyo Mungu aliifanya tu Himaya ya Kirumi kumchukua na kumweka huko nje kisiwani. Ndipo kasema, “Sasa, hima, Yohana, ninataka kukuonyesha jambo fulani litakalotukia.” Mtume wa mwisho, hakukuwako na mwingine wa kuyaandika ila Yohana. Kwa hiyo wakamweka huko nje kwenye kisiwa cha Patimo kutoka mwaka wa 95 A.D. hadi 96 A.D. Naye akaliandika, na kusema:

*Mimi...ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja  
nanyi katika mateso...*

<sup>83</sup> Sasa, yeye hakunena juu ya ile Dhiki Kuu. Hiyo haikuwa ni ile Dhiki Kuu, wala haiji kwa Kanisa. Ile Dhiki Kuu inawajia Wayahudi, si Kanisa. Kwa hiyo haikuwa ni ile Dhiki, ile Dhiki Kuu.

<sup>84</sup> Sasa kifungu cha 10:

*Nilikuwa katika Roho siku ya Bwana, nikasikia  
nyuma yangu, ninii...sauti...ya baragumu,  
nalikuwa katika Roho siku ya Bwana,...*

<sup>85</sup> Sasa huwezi kufanya lolote jema mpaka kwanza uingie katika Roho; Mungu hawezি kukutumia. Wewe ni—wewe ni—wewe ni—wewe ni...Jitihada zako zote ni—ni bure mpaka kwanza ulifanye katika Roho. “Kama nitaimba, nitaimba katika Roho. Kama nitaomba,” Paulo alisema, “nitaomba katika Roho.” Na ndipo kama kuna kitu chochote kitakachonijia ambacho kina faida yoyote, hakina budi kufunuliwa kwangu na Roho na kuthibitishwa kwa Neno (kudhihirishwa kwa matokeo yanayopatikana).

<sup>86</sup> Sasa kama vile, kwa maneno mengine, kama nikisema, Yesu Kristo aliahidi katika Neno Lake ya kwamba kama ningetubu, nibatizwe katika Jina la Yesu Kristo, nitapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Jambo la kwanza nitakalofanya ni kutubu. Imefunuliwa kwangu kwamba hiyo ni kweli. Kisha nibatizwe katika Jina la Yesu Kristo, basi matokeo yake ni: nitapokea Roho Mtakatifu.

<sup>87</sup> Kama nikiwa mganjwa, Naye aliniahidi kama nikiamini na kuwaita wazee wa kanisa wanitie mafuta, waniombee, kuomba kwa imani kutamwokoa mganjwa huyo. “Bwana, ninaamini. Ninafuata maagizo Yako, jalia mzee aniombee, anitie mafuta.” Hilo latosha, endelea tu, ime—imekwisha kabisa.

<sup>88</sup> “Loo,” unasema, wewe, “sioni tofauti yoyote, hata hivyo.” Yesu hakuwa amezaliwa, hapo Mungu alipomchinja kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Yeye alikuwa—Yeye alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyechinjwa kabla ya

kuwekwa misingi ya ulimwengu. Lakini katika nia ya Mungu Mwenyewe, Yeye alikuwa tayari amechinjwa. Wala mimi sikuwa hapa, wala wewe; bali katika kitabu cha Mungu, kama majina yetu yaliwahi kuwa mle, yaliandikwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

<sup>89</sup> Mungu anaposema jambo lolote, halina budi kutukia. Kwa hiyo unapotimiza masharti ya Mungu, kumbuka tu, Mungu atajidhihirisha Mwenyewe na kuyashughulikia mengine, wewe endelea tu, ni kazi iliyomalizika. Loo, hilo si ni la ajabu? Loo, jamani, wazia! Mwambie Mungu tu... Naye Mungu alisema, "Wewe fanya *hivi*, nami nitafanya *hivi*." Vema, kama nikienda nifanye *hivi*, Yeye hana budi kufanya *vile*.

<sup>90</sup> Sasa, ibilisi anasema, "Unaona, Yeye anachelewa."

Hilo halileti tofauti yoyote. Danieli aliomba wakati mmoja na ilikuwa siku ishirini na moja kabla Malaika hajamfikia kamwe, bali hakuvunjika moyo, alijua atakuja kwa vyovyyote *vile*, kwa hiyo alingojea tu mpaka akafika. Wazo ndilo hilo. Loo, hapo ndipo unapata imani. Sasa hatuna budi kuachana na hilo, tungefanya ibada ya uponyaji upesi sana, sivyo? Hiyo ni kweli. Naam, ya imani. Lakini tunataka ibada ya kuiponya nafsi, kuponya upande wa ndani, kwa sababu huo ndio utakaodumu, ukipata Uzima wa Milele. Uzima wa Milele hautoweki wala kuchakaa, unadumu, unadumu *vile*.

<sup>91</sup> Sasa, yeye aliingia katika Roho kabla jambo lolote halijatukia. Jambo la kwanza alilofanya, yeye alikuwa katika kisiwa kiitwacho Patimo (mambo haya yote aliyokuwa amefanya), naye akasema, "Nilisikia sauti," na mambo haya mengine yote. Lakini kabla chochote hakijatukia, yeye alikuwa katika Roho. Na ukiangalia hilo katika Biblia yako, herufi kubwa ya Roho, Roho Mtakatifu. Amina! Aliingia katika Roho. Loo, ninafikiri tu hilo ni zuri sana:

*Nilikuwa katika Roho siku ya Bwana,...*

<sup>92</sup> Siku gani? Siku ya Bwana. Sasa, huo hapo mjadala mkubwa. Hebu tuutulize huo, kwa dakika moja tu.

<sup>93</sup> Sasa, kama tulivyosema asubuhi ya leo, wengine walisema ya kwamba ufunuo, wa Mathayo Mtakatifu 17, ulikuwa "Petro." Kanisa Katoliki liliusema, "Yeye alilijenga Kanisa Lake juu ya Petro; yeye alikuwa papa wa kwanza." Angaliwezaje kuwa papa naye alikuwa ameo? Mnaona? Kisha kasema, "Petro alienda Rumi, akazikwa kule." Basi niambieni mahali pamoja, historia ama mahali popote, ambapo Petro aliwhahi kwenda Rumi. Mnaona? Paulo alienda, bali si Petro. Vema.

<sup>94</sup> Kwa hiyo tunaona ya kwamba itikadi hizi zote na kadhalika, zimeingia tu kisiri. Mnaona? Lakini, na watu siku hizi ni... kila uendako, wao... Kanisa fulani kubwa lina msuamari fulani uliokuwa mkononi Mwake. Mnajua wana misuamari mingapi, misuamari ya kweli, leo hii iliyokuwa katika...? Kumi na tisa.

Wana mifupa, wana—wana vipande vyā majoho, na kugusa na kushika. Nasi hatuna—hatuna vitu hivyo, hatuvihitaji hivyo. Kristo yu hai! Yuko ndani yetu, sio msumari fulani, ama kipande cha msalaba, ama kipande cha mfupa, ama kitu fulani. Yeye ni Mungu aliye hai, akiishi ndani yetu sasa, akijidhihirisha Mwenyewe. Tuna kitu kimoja tu cha ukumbusho, hicho ni Meza ya Bwana, kumbukumbu ya kifo Chake. Lakini kuhusu Kristo Mwenyewe, Yeye yuko pamoja nasi na ndani yetu. Na hicho ndicho kitu tunachotaka kupeperusha (utukufu wa Roho Mtakatifu) kwa ulimwengu. Tuupeperushe mpaka Taa itakapozima. Vema.

<sup>95</sup> Sasa, ninii... Kwa hiyo, mnaona, tulichukua upande huo mwininge wa barabara. Mnajua sikuzote nimejaribu kuwa hivi, na Bwana wetu daima amenifunulia; kuna kupita kiasi upande mmoja, na kupita kiasi upande mwininge, bali papo hapo katikati ya barabara ndipo ulipo Ukweli. Hivi mliona Isaya, ambapo Yeye alisema ya kwamba kutakuwako na njia kuu? Isaya 35. Nanyi mnakumbuka jinsi ndugu zetu Wanazarayo walivyozoea kuimba ule wimbo, mwajua, “*Barabara Kuu ya Utakatifu. Barabara Kuu ya Utakatifu.*” Sasa, kama utasoma Biblia yako vizuri, haisemi “barabara kuu ya utakatifu.” Ilisema, “Kutakuwako na barabara kuu na *njia*, nayo itaitwa,” sio barabara kuu ya utakatifu, bali “*njia* ya utakatifu.” Na ni kiunganishi ambacho kinanimalizia sentensi yako. Mnaona? “Kutakuwako na njia kuu *na* njia, nayo itaitwa *njia* ya utakatifu,” sio njia kuu ya utakatifu.

<sup>96</sup> Mnaona, barabara inajengwa, *njia*... Barabara nzuri inapojengwa, sehemu iliyo juu zaidi iko katikati, kwa sababu inaachilia takataka zote zifagiliwe pande zote mbili. Jambo ndilo hilo. Mtu anapomjia Kristo kweli, yeye ameyaelekeza macho yake kwa Kristo. Kama yeye kidogo ana mihemko, atakuwa mlokole. Kama ni baridi kidogo, ataenda upande huu mwininge na awe tango tu, upande huo mwininge; mnaona, akili zake. Lakini jambo muhimu ni papo hapo katikati ya barabara, ukiwa na Roho wa kutosha ndani yako, anayekupasha joto na unapiga hatua. Amina! Na huku unajua ya kutosha kujidumisha chini ya utiifu kwa Roho, kuenenda kama tu Roho anavyoenenda; sio mpaka wala baadaye, jinsi tu Roho anavyoenenda.

<sup>97</sup> Kanisa Katoliki lilisema, “Ule ufunuo ulikuwa ni Petro.”

Kanisa la Kiprotestanti likasema, “Ulikuwa ni Kristo.”

Bali Biblia inafundisha, “Ulikuwa ni ule Ufunuo aliompa (Mungu alimpa) wa Kristo.”

“Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

“Heri wewe Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havijakufunulia hili, hakuna mtu, seminari, wala nyumba ya watawa, chochote kile, kilikufundisha Hili. Bali Baba Yangu

aliye mbinguni amekufunulia hili. Wewe ni Petro, juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, wala malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

<sup>98</sup> Sasa tunafikia mahali pengine hapa ambapo wanapata mawazo mawili mbalimbali. Sasa, huenda nimekosea; kama nimekosea, Mungu anisamehe. Lakini sitakubaliana na Waadventista wa Sabato wanaosema ya kwamba, “Ilikuwa ni siku ya saba alipokuwa kule, siku ya Bwana.” Ndugu Waadventista wa Sabato, na wengi wao, wanadai ya kwamba ilikuwa ni siku ya sabato ambayo aliita siku ya Bwana. Kanisa la Kikristo linaiita, siku ya Bwana, “Ju—Jumapili, siku ya kwanza.” Nasi tunaona mara nyangi ya kwamba—ya kwamba kanisa la Kikristo bado, hata wa leo, Waprotestanti, wanaiita “Siku ya Bwana, Jumapili.” Hilo si la kimaandiko. Jumapili ilikuwa ni siku ya kwanza ya juma katika Biblia, si siku ya Bwana. Wala haikuwa ni siku ya saba, sabato. Hainingeweze kana kuwa mojawapo ya siku hizo maana ilimchukua Yohana miaka miwili kuandika Ufunuo. Ilikuwa ni siku gani? Kungekuwa na nyangi ya hizo siku za saba na siku za kwanza ambazo zingepita.

<sup>99</sup> Biblia, Ufunuo kiliandikwa kuanzia mwaka wa 95 A.D. hadi 96, miaka miwili. Ilikuwa ni siku ya Bwana. Siku ya Bwana ni vile hasa ilivyosema, na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Yohana alibebwa katika Roho akafika kwenye siku ya Bwana. Hii ni siku ya mwanadamu, bali siku ya Bwana itakuja. Kote katika Maandiko tutapata ya kwamba ye ye alikuwa katika siku ya Bwana, alitwalisha katika roho na kuchukuliwa kupelekwa kwenye siku ya Bwana. Amina! Hiyo ni kweli. Mnaona, alikuwa katika siku ya Bwana. Biblia inazungumza juu ya siku ya Bwana. Tutaifikia katika muda kidogo, Maandiko mengi.

<sup>100</sup> Jambo la kwanza, siku ya sabato, kama tunavyoizungumzia, siku ya sabato sio kutunza siku fulani. Hatuna amri ya kutunza Jumamosi kama sabato. Hatuna amri ya kutunza siku ya kwanza kama sabato, katika Agano Jipy. Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 4, “Kama Yesu angaliwapa raha, asingenena juu ya siku nydingine baadaye.” Hiyo ni kweli. Lakini imesalia raha, ama kutunza sabato, kwa watu wa Mungu. Kwa kuwa sisi tulioamini, pia, tumeingia katika raha Yake; tunaacha kazi zetu kama Mungu alivyocha Zake.

<sup>101</sup> Angalieni! Loo! Bwana asifiwe. Ninaanza tu kujisikia vizuri sana, ninajisahau.

<sup>102</sup> Angalia, katika siku ya sabato. Mungu aliumba dunia katika siku sita, kisha siku ya saba akaingia katika raha wala hakurudi tena kujenga dunia zingine. Ndipo akawapa watu kama kumbukumbu. Kwa sababu msingeweza kuiweka sasa, maana wakati mkiweka sabato hapa, upande ule mwingine wa ulimwengu ni Jumapili tena basi. Mnaona? Kwa hiyo ilionyesha ya kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya watu fulani, kipindi na wakati

kwa ajili ya Israeli. Lakini basi imesalia kuweka sabato kwa ajili ya watu wa Mungu.

*Kwa maana sisi... tulioamini tunaingia katika raha Yake... ijapokuwa zile kazi... (Ninanukuu Waibrania, mlango wa 4)... ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.*

*Kwa maana alinena mahali fulani... hivi, ...siku ya saba...*

*Na tena, ameweka siku fulani, akisema katika Daudi, ... (ninyi mnaoliandika, Waibrania 4)*

*Tena, aliweka siku fulani, akisema katika Daudi, Leo, baada ya muda mwingi namna hii; imesikiwa, Mkisikia... ama kasema, Wakati mkiisikia sauti yake, msiuifanye mgumu moyo wenu.*

*Kwa maana kama Yesu angaliwapa raha (siku)... asingaliineni siku nyininge baadaye.*

Lakini imesalia... raha (ama kuweka sabato)...

<sup>103</sup> Neno “raha.” Sabato ni neno geni kwetu, ambalo maana yake ni “raha.” Ni neno la Kiebrania ambalo linamaanisha siku ya “raha,” siku ya sabato; usifanye kazi, pumzika.

*Kwa maana kama Yesu angaliwapa raha,... asingalininii... asingalizungumzia siku nyininge.*

Lakini imesalia... raha (ama kuweka sabato) kwa watu wa Mungu.

*Kwa maana sisi ambao tumeingia katika raha yake,... tunastarehe katika kazi... zetu, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi yake.*

<sup>104</sup> Kamwe hatuirudii kesho yake juma lijalo na kuanza tena, tumeingia katika Raha. Yesu akizungumza juu ya zile heri, alisema, “Mmesikia watu wa kale wakisema, ‘Usiue.’ Nawaambia, mtu yejote, kumkasirikia ndugu yake pasipo sababu, ameua tayari. Mmesikia ikisemwa, hao wa kale, ‘Usizini.’ Hiyo ndiyo amri. Lakini nawaambia, kila amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Hiyo ni kweli?

<sup>105</sup> Kwa hiyo mambo haya yote yalikuwa ni kumbukumbu, ishara tu, maajabu, yakiungojea wakati ulio halisi kuja. Sasa, Yesu alipomaliza hayo, Mathayo 11, (zile heri) Yeye alisema:

*Njoni Kwangu, ninyi nyote mnaosumbuka, mliochoka, na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitawapa raha nafsi mwenu.*

*Jitwikeni nira yangu mimi, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekemu wa moyo... (hiyo ni kweli?)*

*Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na... kulemewa na mizigo, nami nitawapa raha nafsini mwenu.* (“Kama mmesumbuka siku moja, siku kumi, miaka mitano, miaka thelathini na mitano, miaka hamsini, miaka tisini, nanyi mmechoka na kudhoofika, njoni Kwangu, nitawapa Raha. Nitawaondolea mziguo wote wa dhambi, na kuingia ndani yenu, na kuwapa raha kamilifu na utoshelevu.”)

<sup>106</sup> Sasa, hiyo raha ni kitu gani? Hebu—hebu tulitatue hili kidogo, tuone kwamba ni nini. Baadhi yao walisema, “Mbona, wewe nenda kajunge na kanisa.” La! “Liandikishe jina lako kitabuni.” La! “Vema, namna fulani ya ubatizo wa maji.” La! Hebu na tulitatue tuone kwamba ni kitu gani. Mngetaka kufanya hivyo papa hapa wakati tukingojea? Tutaona mahali Yohana alipoenda. Yeye aliingia kwenye siku ya namna gani?

<sup>107</sup> Wakati Yesu alipokufa duniani, na kazi Yake ikamalizika, Yeye aliingia mahali fulani.

<sup>108</sup> Sasa hebu turudi kwenye Isaya mlango wa 28, na kifungu cha 8. Ninaamini ndipo, sasa, Isaya 28:8. Basi na tusome, Isaya 28, nabii huyo akinena miaka mia saba na ishirini kabla hajatukia. Sasa, ni wangapi wangetaka kujua *sabato* ya kweli ni ipi, raha ya kweli? Hii hapa. Sasa, hapa ndipo nabii aliponena habari zake, nami nitawaonyesha mahali ilipotimia. Angalieni, Isaya 28:8:

*Maana zote... (nabii akitabiri juu ya siku hizi)*

*Maana meza zote zimejaa matapiko na uchafu,* (watu wakila ushirika, ambao huvuta sigara na kunywa pombe na kusema uongo na kuiba)...*hata hapana* mahali safi.

*Atamfundisha nani maarifa?...*

Ungemfundisha nani maarifa siku hizi?

<sup>109</sup> Ni wangapi waliomsikia Billy Graham leo? Yalikuwa ni mahubiri mazuri sana aliyohubiri, jinsi ambavyo watu wangeweza kuamini uongo na kuendelea na uongo huo na—na hata kujihesabia haki na kufikiria kwamba walikuwa wakifanya haki. Umma wa Marekani ukichukua, yeye alisema, na kusema, “Chujio la mtu mwenye busara, na sigara ya mvuta sigara,” wakichukua moja ya uongo wa ibilisi, na badala ya kumfanya mjinga, vyovyyote alivyo, kuvuta kitu kama hicho na kujaribu kumfanya yeye mtu mwenye busara. Yeye ni mpumbavu hata kuivuta, wakati ninii... wakati imejaa mauti na kansa na kila kitu kingine, naye angali anaivutia ndani ya mapafu yake. Yeye ni mpumbavu. Sio ninii—sio chu—chujio la mtu mwenye busara, wala hakuna kitu kama hicho. Mtu mwenye busara hatumii kitu hicho.

<sup>110</sup> “Hakuna maisha ila kwenye Oertel ya 92,” ama kitu kama hicho. Hakuna Uzima nje ya Kristo, huo ndio Uzima halisi wa

kweli. Ni kitu gani kinachowafanya wanaume na wanawake wanywe kitu hicho? Kwa sababu wanajaribu kuridhisha hicho kitu mle ndani ambacho Mungu alikiweka mle ndani wapate kumwoneea Yeye kiu, nao wanajaribu kukiridhisha kwa mambo ya ulimwengu huu. Na hiyo ndiyo sababu tuna vitu hivyo. Hiyo ndiyo sababu watu wanatenda jinsi hiyo, kwa maana wanajaribu kuridhisha hicho kiu kilicho ndani yao kwa ajili ya Mungu, naye ibilisi anawapa mauti badala ya Uzima.

*...meza zote zimejaa matapiko...*

<sup>111</sup> Makasisi, kila kitu kingine, wananaena habari zake, “Ni sawa kufanya burudani ndogo safi.” Hakuna kitu kama hicho!

*Atamfundisha nani maarifa? na ni nani atakayemfahamisha...habari hii? ni wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini.* (Sasa sisi si watoto wachanga tena.)

*Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huko kidogo:*

*Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa;*

*Ambao aliwaambia, Hii ndiyo... (ati nini? kuweka sabato!)...raha yenu, ambapo mnaeweza kumfanya aliyechoka... (“Njoni Kwangu ninyi mlionchoka na mumelemewa na mizigo mizito.”) ...mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika: lakini hawangesikia.*

<sup>112</sup> Hilo lilitukia lini? Miaka mia saba na kumi na miwili baadaye wakati kwenye Siku ya Pentekoste midomo ya watu wageni iliwashukia watu nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu na kuanza kunena kwa lugha zingine na, Roho Mtakatifu akayachukua maisha yao mateka, wakaachana na mambo yao ya kilimwengu. Ndipo wakaingia katika Raha pamoja na Kristo. Paulo alisema, katika Waembrania mlango wa 4, “Sisi tulioingia katika raha Yake tumeachana na matendo yote ya kilimwengu kama Mungu alivyofanya kwenye ile siku ya uumbaji Wake, alilingia katika raha Yake, nasi tunaingia pamoja Naye baada ya kuachana na kazi zetu za ulimwenguni.” Hiyo hapo Sabato yenu halisi, ya kweli.

<sup>113</sup> Kwa hiyo Paulo alitwaliwa na kuingia kwenye huyo Roho wa Sabato, naye akahamishwa na Roho Mtakatifu mpaka akaingia kwenye siku ya Bwana.

<sup>114</sup> Ni kwa nini tuna vita? Ni kwa nini tuna taabu? Ni kwa nini taifa linapigana na taifa? Yesu alikuja, Mfalme wa Uzima, nao wakamwua.

<sup>115</sup> Katika majuma machache, ama hata sasa hivi, kuna kulungu na akina Baba Krismasi na—na milio ya kengele na kila namna

ya vitu vikining'inizwa, ambayo ni sherehe ya kipagani. Ni kanuni ya kanisa Katoliki. Watu wakilipa gharama kubwa na kubadilishana zawadi na vitu kama hivyo, upagani! Krismasi ni siku ya kuabudu.

<sup>116</sup> Na jambo lingine, wala Kristo hakuzaliwa tarehe ishirini na tano Desemba. Isingeweze kana Kwake. Kama ulipata kuwa Uyahudi, vilima vimejaa theluji, vibaya sana kuliko ilivyo hapa. Alizaliwa Aprili wakati maumbile yote yanapochipusha.

<sup>117</sup> Sasa, bali ni mapokeo yao. Na ni kwa nini—kwa nini tunafanya mambo hayo? Ni kwa sababu tunafuata mapokeo ya wanadamu badala ya amri za Mungu. Hao... Kitu kama hicho kisingejalisha, bali wanaifanya tu kuwa ni siku ya biashara. Ni fedheha, aibu kwao kufanya vitu kama hivyo. Sherehe ya kipagani! Ni lini Baba Krismasi alipata kuwa na uhusiano wowote na Yesu? Ni lini sungura wa Pasaka ama kuku ama... walioitiwa rangi kwa namna fulani ya wino ama chochote kile, ama namna fulani ya sungura mdogo mweupe walipata kuwa na uhusiano gani na kufufuka kwa Yesu Kristo? Hivi hamwoni jinsi ulimwengu wa kibiashara...?

<sup>118</sup> Hiyo ndiyo sababu wanauzu maskini vitabu hivi vyatoki, na picha chafu, na vinyaa, na vitu kama hivyo, ni kwa sababu asili ya watu inatamani sana upuzi kama huo. Ni kwa sababu kuna kasoro moyoni, hawajawahi kuingia katika Raha hiyo pamoja na Mungu na kuachana na mambo haya. Wanapoingia kwenye hiyo na kumpokea Roho Mtakatifu, basi wamemalizana na ulimwengu na mambo ya ulimwengu.

<sup>119</sup> Mungu alimhamisha. Loo, siamini ya kwamba alichukuliwa kama Paulo, sasa, huko juu mpaka mbingu ya tatu na kuona mambo. Vema, Roho Mtakatifu wa thamani alifanya hivyo majuma machache yaliyopita, hapa, akaniruhusu kuona... Kwa maneno mengine, nilikuwa ninaogopa mauti, ndipo Roho Mtakatifu akanichukua na kunionyesha jinsi ilivyokuwa. Mmeusikia ushuhuda huo. Ndipo niliporudi, "Basi, mauti, uko wapi mwiba wako?" Kuhamishwa kuona yale yaliyokuwako ng'ambo ya pazia. Aliniruhusu kurudi kuwaambia ya kwamba huko ng'ambo sisi si mizuka na pepo, sisi ni wanaume na wanawake, vijana, hatutakuwa kamwe, hatutakuwa wagonjwa, ng'ambo tu ya pazia. Mauti hayawezi kufanya zaidi ya kukuvuta kukuungiza Mahali pale.

<sup>120</sup> Sasa, Yohana alihamishwa kutoka kwenye kisiwa cha Patimo, katika Roho, mpaka kwenye siku ya Bwana. Hii ni siku ya wanadamu, wanadamu wanapigana, bali siku ya Bwana itakuja wakati falme hizi zitakuwa ni falme za Bwana wetu na za Kristo Wake, ndipo kutakuwako na ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Siku ya Bwana, siku ya kuja Kwake, hukumu Yake, hiyo itakuwa ndiyo siku ya Bwana.

<sup>121</sup> Hii ni siku ya wanadamu, hiyo ndiyo sababu wanakusukuma-sukuma kila mahali na kukufanyia wapendavyo, bali kutakuwako na wakati... Wanakuita... wanakuita sasa, "mtakatifu anayejibingirisha na mlokole," bali utakuja wakati, unaona, ambapo hawatafanya hivyo. Watalia na kuomboleza na kuanguka miguuni pako. Biblia ilisema, katika Malaki 4, hata mtatembea juu ya hayo majivu wakiisha kuteketezwa; halitawaachia shina wala tawi. Hivyo ndivyo Biblia inavyosema hasa, "Wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu." Hiyo ni kweli kabisa. Hawatasalia shina wala tawi, hakuna kitu cha kurudia. Nao wataangamizwa kabisa. Sasa hii ni siku ya mwanadamu (matendo ya mwanadamu, kazi za mwanadamu, kanisa la mwanadamu, mawazo ya mwanadamu), bali siku ya Bwana inakuja.

<sup>122</sup> Sasa, ye ye alikuwa katika Roho katika siku ya Bwana. Vema, na jambo la kwanza alilosikia alipokuwa katika Roho katika siku ya Bwana... Sasa tumefika kwenye kifungu cha 10:

... *katika Roho siku ya Bwana*, naye akasikia *sa-...*  
*sauti, ... kama ... ya baragumu,*

<sup>123</sup> Hebu tusipite mfano mmoja, sasa. Kama itatubidi kulichukua kesho, tunaweza kulichukua, mnaona. Mtu fulani aingalie tu saa ya ukutani, nisije nikawachelewesha.

<sup>124</sup> Vema, sasa, "... nilikuwa katika Roho katika siku ya Bwana." Sasa kumbukeni, jambo la kwanza likupasalo kufanya ni nini? Ingia katika Roho. Funuo hizi zitapataje kuwajia kamwe? Ingieni katika Roho. Utampataje Roho Mtakatifu kamwe? Ingia katika Roho. Ingia katika Roho!

<sup>125</sup> Ulipokuwa mwenye dhambi na ukaenda kwenye dansi, uliingia katika roho *hiyo*. Loo, jamani, ulianza kupiga makofi yako na kufanya vishindo kwa miguu yako na vifijo, na kuitupa kofia yako sakafuni, na kuzunguka na kuzunguka, ukitenda kipumbavu. Ulikuwa katika roho yake. Ungeweza kuwazia jamaa, aliyekuwa shabiki wa dansi, akienda kwenye dansi, aseme, "Vema, ninyi nyote mna wakati mzuri, nadhani."

"Loo!" wangesema. "Ewe ua la ukutani, ondoka hapa!"  
 Mnaona?

<sup>126</sup> Uende kwenye mchezo wa mpira, mtu fulani aingize goli, ama chochote kile, uketi na kuangalia, na kusema, "Vema, nadhani hilo lilikuwa zuri sana." Hasha, usingekuwa shabiki wa besiboli, usingekuwa ninii halisi... usingekuwa katika roho ya besiboli. Mtu anapoingiza goli, unainuka na kupiga makelele, "Whiu! Jamani! Ushindi!" Uipige kofia ya mtu fulani kutoka kichwani mwake namna *hiyo*, hakuna mtu atakayesema neno kulihusu.

<sup>127</sup> Halafu kanisani unapoingia katika Roho, unasimama na kupiga makelele, "Utukufu! Haleluya! Bwana asifiwe!"

Mtu fulani anageuka, kasema, “Mtakatifu anayejibingirisha.” (Loo, Ndugu Wood...)

<sup>128</sup> Nitawaulizeni swalii. Kama sisi ni watakatifu wanaojibingirisha kwa sababu tunafanya hivyo, basi wao ni *waovu*- wanaojibingirisha huko nje. Afadhalii niwe mtakatifu anayejibingirisha (Nawe je?) kuliko asiye mtakatifu. Jamani! Hakika! Hao *waovu*-wanaojibingirisha.

<sup>129</sup> Sasa, ye ye alikuwa katika Roho. Aliingia katika Roho, ndipo mambo yakaanza kutukia. Ndipo basi wakati alipofika kule, alisikia baragumu. Sasa, baragumu sikuzote hutangaza kukaribia kwa kitu fulani. Kama wakati unapokuja... M—mfalme anapokaribia, watapiga baragumu. Yesu atakapokaribia, atapiga baragumu. Hiyo ni kweli? Wakati Yusufu alipotokea, walipiga baragumu. Na sasa kitu fulani kinatokeza, Yohana aliingia katika Roho na kusikia baragumu. Alisikia baragumu, naye akageuka kuangalia kilichokuwa nyuma yake aliposikia baragumu; akiisha kuingia katika Roho.

<sup>130</sup> Labda alikuwa akicheza, akiruka, akikimbia huku na huku kisiwani. Alikuwa na wakati mzuri, alikuwa katika Roho. Kwa hiyo, basi ye ye... Hilo linawenza kusikika la kukufuru, bali silimaanishi hivyo, mnaona. Angeweza! Hiyo ni... vema, huenda alikuwa akifanya hivyo. Ninaamini alikuwa na wakati mzuri katika Roho, akimsifu tu Mungu, kwa sababu hilo hasa ndilo lililotukia hapo Roho alipowashukia mara ya kwanza. Roho Mtakatifu alipowashukia, waliyumbayumba kama wanaume na wanawake walevi, na kufanya kama walevi, na kupayuka-payuka. Na kuita-... kuendelea jinsi hiyo hata watu wakasema, “Watu hawa wamejaa mvinyo mpya.” Hivyo ndivyo walivyotenda mara ya kwanza, kwa hiyo huyo Roho akija tena, labda atafanya vivyo hivyo. Mnaona? Hakuna mapya kuhusu jambo hi—hili, hii ni dini ya *mtindo wa kale*. Naam.

<sup>131</sup> “Katika Roho siku ya Bwana.” Sasa, tunalisiikia. Kitu gani sasa? Sasa, ye ye alikuwa akifanya nini? Alihamishwa kutoka kwenye kisiwa hicho sasa, katika Roho, akaingia kwenye siku ya Bwana. Na mara alipofika kwenye siku ya Bwana, alisikia baragumu. Ni kitu gani? Ni Mtu anakaribia. Mtu mashuhuri anakaribia. Baragumu inalia, mtu Fulani anakuja! Akaangalia! Haleluya! Baragumu:

*Ikisema, Mimi ni Alfa na Omega, wa kwanza na wa mwisho:... (si tangazo la mtu wa pili ama mtu wa tatu, bali Mtu wa pekee)... Mimi ni wote wawili Alfa na Omega, ... (“Kabla sijakuonyesha chochote, ninataka kukujulisha mimi ni Nani!”)*

<sup>132</sup> Ufunuo ulio mkubwa kuliko zote ni wa Uungu, Uungu Mkuu wa Bwana wetu Yesu Kristo. Huwezi kuingia kwenye msingi wa kwanza mpaka utakapoamini huo, kutoka nje... Hivyo ndivyo Petro alivyo sema, “Tubuni, kisha muuone Uungu. Mkabatizwe

katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, ndipo mko tayari kuingia katika Roho.” Jambo la kwanza likupasalo kujua ni Uungu wa Kristo. “Mimi ni Alfa na Omega! Mimi ni kuanzia A hadi Z, hakuna mwingine ila Mimi. Nilikuwako hapo mwanzo, nitakuwako huko mwisho. Mimi ni Yule aliyekuwako, aliyeleo, na atakayekuja, Mwenyezi.” Wazieni Hilo! Hivyo ndivyo baragumu ilivyosema.

<sup>133</sup> Kuwa mwangalifu Yohana! Umeingia katika Roho, kitu fulani kitafunuliwa kwako. Ni kitu gani? Baragumu ililia, jambo la kwanza, “Mimi ni Alfa na Omega.” Wa kwanza wa funuo zote. (Loo, ewe mwenye dhambi, inama, tubu sasa kabla wakati haujachelewa sana.) “Mimi ni Alfa na Omega.” Hilo ndilo jambo la kwanza alilomjulisha, kwamba Yeye ni nani. (Ni nani huyu anayekaribia? Je, huyu ni Mfalme Yesu? Mfalme Mungu? Mfalme Roho Mtakatifu?) Alisema, “Mimi ni hao wote! Mimi ni kuanzia A hadi Z. Mimi ni mwanzo na mwisho. Mimi ni wa Milele, Asiyepatikana na mauti!”

<sup>134</sup> Baadaye kidogo tu tunamwona katika utu wake wenye sehemu saba, angalia kile alichoso basi. “Mimi ni mwanzo na mwisho. Mimi ni Alfa na Omega, wa kwanza na wa mwisho. Nilikuwa kabla hapajakuwapo na wa kwanza; na baada ya kutokuwa na wa mwisho tena, bado nitakuwepo,” kwa maneno mengine. “Wa kwanza na wa mwisho!”

...na, *Uyaonayo*, andika katika kitabu, na  
upeleke...kwa makanisa saba yaliyoko Asia;  
kwa Efeso,...Smirna,...Pergamo,...Thiatira,...  
Sardi,...Filadelfia, na Laodikia.

<sup>135</sup> Sawa, wa kwanza wa funuo zote ni Uungu Mkuu wa Yesu Kristo. Lazima ujue Yeye ni nani wakati ukisikia Sauti. Sawa, Sauti ile ile iliyosikika juu ya Mlima Sinai, Sauti ile ile iliyosikika juu ya Mlima wa Kugeuka Sura, Yule yule, “Mmoja kama Mwana wa Adamu.”

<sup>136</sup> Sasa angalia katika kifungu hiki kinachofuata. Sawa:

*Nikageuka*... (Mlango wa 12 sasa.)

<sup>137</sup> Tutayaacha makanisa haya kwa dakika moja tu, kwa sababu juma hili zima linakuja kwenye makanisa haya. Mnaona, kwa hivyo tutayapita tu hayo.

<sup>138</sup> Lakini akasema, “Hizi...Nitakuelekeza utume Ujumbe huu ambaeo ninakuonyesha.” Ni nani? “Mimi ni wa kwanza na wa mwisho. Mimi Ndimi Mkuu. Mimi Ndimi Mwenyezi. Na nimekuja kukwambia kuwa ninakupa Ujumbe kwa makanisa saba. Nataka uuandike, uutayarische.” Unaona? “Na makanisa saba yaliyoko Asia.” Sasa, yaliyoko saba makanisa huko wakati huo yenye asili ndani yao ambayo iliwalishwa hizi nyakati za kanisa zijazo.

<sup>139</sup> Sasa:

*Nikageuka ili niione sauti iliyosema nami. Nikageuka, nikaona vinara vya mishumaa saba vya dhahabu;*

<sup>140</sup> “Vinara vya mishumaa saba vya dhahabu.” Sasa, ni . . . Toleo la King James, ambapo labda unalo la Scofield au—au labda la Mfuatano wa Thompson, au baadhi yao, si sahihi hapo. Haisemi vinara vya mishumaa, inasema vishikizo vya taa; vinara vya taa, naamini, ndilo neno sahihi, neno sahihi lililosemwa katika tafsiri ya asili. Tazama, kwa maneno mengine, vinara hivi vya taa saba vya dhahabu vilikuwa makanisa saba. Yeye anasema baadaye kidogo, ninii . . . katika kifungu cha 20 hapa, “Vinara saba vya taa uliviyoviona ni makanisa saba.” Kwa hiyo, mnaona, kama ulikuwa ni mshumaa, karibuni ungetumika na kumalizika, kwa muda mfupi tu. Bali si mishumaa, ni ki—kinara cha taa. Inasema ni kinara cha taa. “Nilipogeuka niliona mtu kama Mwana wa Adamu amesimama katikati ya . . . katikati ya vinara vya taa saba.”

<sup>141</sup> Sasa—sasa angalieni. Mshumaa karibuni ungeungua, nao ungezima, hakungekuwako na cha zaidi, katika saa chache ungeungua uishe. Lakini kinara cha taa, kinara cha taa ni kama hiki, . . .

<sup>142</sup> Hapa, hebu—hebu tuchukue Maandiko hapa, hebu—hebu tufungue Zekaria 4:1, basi labda tunaweza kupata katika Zekaria hapo kile tunachotaka. Zekaria 4:1, nami ninaamini basi labda katika hili tutaweza ku—kuvuta pamoja kile tunachotaka. Siwezi kupata Zekaria katika Zefania, sivyo? Vema. Vema. Maskini Biblia yangu ya kale karibu imechakaa. Zekaria 4:1, sikilizeni kwa makini sasa, mpate picha nzuri hapa:

*Na yule malaika . . .*

<sup>143</sup> Nabii, sasa, miaka mia tano na kumi na tisa tu kabla ya Kristo:

*Na yule malaika aliyesema nami akanijia mara ya pili, akaniamsha, kama mtu aamshwavyo katika usingizi wake, (Sasa nabii huyu yuko katika ono.)*

*Ndipo yeye akaniuliza, Unaona nini? Nikasema, Nimeona, na tazama, kinara cha mshumaa . . . (Sasa, hilo ni neno lile lile lililotafsiriwa kinara cha taa.) . . . cha dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu . . . juu yake, (Hiyo ilikuwa ni taa.) . . . na taa zake saba juu yake, tena iko mirija saba ya kuleta mafuta kwa taa zote zilizo juu yake: (Mnaona, nyakati zile zile za kanisa zikija. Mnaona?)*

*Na mizeituni miwili karibu yake, . . . (Sasa, ni aina gani ya . . . Walitumia nini kwenye taa hizo katika wakati wa Biblia? Kuna mtu anayejua? Mafuta. Ni mafuta ya aina gani? Mafuta ya mizeituni.) . . . mizeituni miwili . . . (Ni kitu gani? Agano Jipywa na la Kale; miwili iliyosimama*

*karibu yake.) . . . moja upande wa kuume wa lile bakuli, na mmoja upande wake wa kushoto.*

Nami *nikajibu, nikamwambia yule malaika aliyesema nami, nikasema, Ee bwana wangu, vitu hivi ni nini?*

*Ndipo malaika aliyesema nami akajibu, akaniambia, Hujui vitu hivi—hivi ni nini? Nikasema, La, bwana wangu.*

*Ndipo akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la BwANA kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema BWANA wa majeshi.* (Yeye ataufanya upya Yerusalem.)

<sup>144</sup> Sasa, kinara cha mshumaa ni nini? Ni kinara cha taa. Basi hebu ona jinsi lilivyo la kupendeza. Hapa, alipogeuka, alimwona Huyu anayefanana na Mwana wa Adamu hapa amesimama katikati ya vinara vytaa saba vytaa dhahabu, ambalo linamaanisha nyakati saba za kanisa zijazo. Na kila mrija, ama—ama kinara cha taa, kimeshikamanishwa kwenye chetezo kikubwa cha mafuta. Na katika mafuta haya kukatokea taa ndogo yenye umbo la kipekee iliyokuwa na utambi ndani yake nao utambi huo ukanning’inia kwenye hayo mafuta. Na almuradi . . . Walimwaga mafuta juu ya hicho kinara, ambayo yaliujaza ule mrija mkubwa, na lile tawi kubwa, nayo yakaingia kwenye mashina, namna hii. Nayo taa iliyokuwa na utambi ulioning’inia chini, m—mrija huu ulioingizwa katika . . . iliendelea kuwaka, usiku na mchana. Haikukubidi kuiwasha, kamwe haikuzimika; waliendelea tu kumwaga mafuta kwenye huo mrija mkubwa. Navyo vinara hivi vytaa vilivyotokeza namna hii, vilikuwa na taa zimewekwa juu yake. Utambi kutoka kwenye hiyo taa uliingia hapa, ukapata uhai wake kutoka hapa. Loo, ni tofauti jinsi gani na mshumaa. Ni tofauti jinsi gani! Ni kinara cha taa, nacho kinayavuta mafuta.

<sup>145</sup> Sasa, vinara hivi vytaa, moto uliokuwa katika vinara hivi vytaa katika Agano la Kale. Walipoiwasha taa moja, wasingeweza kuiwasha taa ya pili kwa moto ule ule waliokuwa nao mkononi mwao. Waliiwasha taa moja, kisha wakaichukua na kuiwasha taa nyingine, kisha wakaiweka chini. Kisha wakaiwasha taa hii, halafu wakaichukua na kuiwasha taa hii kwa moto ule ule walioanza nao tangu mwanzo. Loo, natumaini halitapita juu ya kichwa chenu. “Yesu Kristo yeeye yule jana, leo, na hata milele,” moto ule ule (Roho Mtakatifu) uliwasha kila moja ya makanisa hayo kote katika nyakati.

<sup>146</sup> Hivi Yesu hakusema katika Yohana 15, “Mimi ndimi mzabibu, ninyi ni matawi”? Sasa, Yeye ndiye Mzabibu mkubwa, sisi ni matawi. Sasa, mzabibu hauzai matunda . . .

<sup>147</sup> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kwamba unaweza kuchukua mti wa jamii ya mchungwa, kama mchungwa, nawe unaweza ku—kung’oa ta—tawi lake, vema, ningesema,

mbalungi, na kuchana mahali padogo kwenye mchungwa huo na kuupandikiza huo mbalungi humo, utakua. Hebu nenda hapa na kuchukua tawi la mlimau na kulipandikiza katika mchungwa, litakua. Ama chukua komamanga, na ulichukue. Ama tunda lolote jamii ya chungwa, chenza ama kangaja, lolote la hayo matunda jamii ya chungwa, na kulipandikiza kwenye mti huu, basi litastawi kwa uhai wa mchungwa; lakini halitazaa machungwa. Litazaa balungi, litazaa kangaja, litazaa malimau, bali linastawi kwa uhai wa mzabibu halisi, bali kama mzabibu huo ukiwahi kuzaa mzabibu mwingine... tawi lingine, litakuwa la uhai ule ule ulio ndani yake, litazaa chungwa. Kwa sababu, hapo mwanzo, kwenye shina lake kuna uhai wa mchungwa, lakini mingine inaweza kuishi kwake almradi ni asili ya jamii ya mchungwa. Bali hauwezi kuzaa tunda la ule wa asili, kwa kuwa si wa asili.

<sup>148</sup> Hivyo ndivyoo kanisa lilitivo. Wameuchana Mzabibu na kupandikiza Presbiteri, Methodisti, Baptisti, na kadhalika namna hiyo. Unazaa tunda la Kibaptisti, tunda la Kipresbiteri, tunda la Kimethodisti, bali kama ukipata... mti huo ukipata kuzaa tawi lingine, litakuwa ni tawi la aina ile ile ulilozaa kwenye Siku ya Pentekoste: Tawi asilia! Litanena kwa lugha na kuwa na nguvu na ishara za Kristo aliyefufuka ndani yake. Kwa nini? Maana linastawi kwa rasilimali asilia lililopandiwa. Kwa kweli, halikupandwa ndani yake, lilizaliwa mle! Bwana asifiwe! Loo, jamani! Sikuliwazia hilo papo hapo.

<sup>149</sup> Mnaona, hii mingine imepandikizwa; wanaipandikiza kwenye mti, kwa hiyo inazaa tunda kwa jinsi yake. Haiwezi kuchukua *Hili*. Haiamini *Lile*, kwa sababu haikujua lolote kulihusu. Lakini kama ikizaliwa katika Uzima ule ule uliotoka kwenye mti huo, hicho ndicho kitu pekee inachowenza kuzaa, ni Uzima wa shina asilia.

<sup>150</sup> Vinara hivi vyote vya taa vinaenea kwenye hilo bakuli moja kubwa, chombo kimoja kikubwa mno, na ninii tisa mbalimbali... ama vinara vya taa saba mbalimbali vinatoka kwake. Na vilipotoka, kila moja ya hizo taa ilikuwa ikituwa kutoka kwenye rasilimali kuu ya maisha yake. Na nuru yake ilikuwa ni kwa sababu mshumaa wake uliingizwa ndani ya mtungi huu mkubwa. Loo, ni picha nzuri jinsi gani ya moja ya hizo nyota saba (kiliwakilisha hizo) maisha yake yakiwa na moto wa Roho Mtakatifu hapa. Nayo... Kwa imani anawaka kwa Roho Mtakatifu, na maisha yake ni taa, ama siyo taa, bali ni utambi uliotumbukizwa katika Roho Mtakatifu (ndani ya Kristo), na kupitua huo utambi inaunyonya Uzima wa Mungu apate kulipa Mwangaza kanisa lake. Loo, ni picha ya namna gani ya mwaminio wa kweli! Ni Nuru ya jinsi gani anayotoa? Nuru ile ile iliyokuwako wakati taa ya kwanza ilipowashwa.

<sup>151</sup> Wakati wa kwanza wa kanisa ulipoanza, ulikuwa ni Efeso. Paulo, yule malaika wa kanisa hilo, mmoja wa zile nyota. Kuna

nyota saba ambazo zinamaanisha malaika saba, "wajumbe" saba. Juma hili ninaweza kuyachukua Maandiko na historia na kuwathibitishia kila mmoja wa hao ni wa kweli katika kila malaika, na kila malaika alikuwa na Nuru ile ile. Hiyo ni kweli. Na halafu moja kwa moja kati ya nyakati hizi, yule Mkuu atakayekuja.

<sup>152</sup> Angalieni, sasa zinavuta kutoka kwenye mtungi huu mkubwa wa Mafuta, ile Nuru...maisha yamezamishwa ndani ya Kristo. Wewe umekufa, na uhai wako umefichwa ndani ya Kristo kwa njia ya...ama yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, na kutiwa Muhuri na Roho Mtakatifu. Hakuna njia hata kidogo ya kukuondoa pale. Unawezaje kuondoka? Hakuna mtu anayeweza kukuchezea. Ncha ya maisha yako inawaka kwa Roho Mtakatifu; loo, inawaka, ikitoa Nuru. Ncha hiyo nyingine ya maisha yako imezamishwa wapi? Katika Kristo. Umekufa na kufichwa katika Kristo, Roho Mtakatifu, anayafungia pale hata unawenza...ibilisi hawezu kukugusa. Amina! Yeye anaweza kuvuma na kufanya makelele. Hata mauti yenyehe hayawezu kukugusa, "Ewe mauti, u wapi mwiba wako? U wapi ushindi wako? Mungu ashukuriwe atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

<sup>153</sup> Mwisho wa kifungu hiki, hebu tukisome:

... *Nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu;*

... *Na katikati ya vile vinara vya taa saba vya dhahabu  
mtu kama...Mwana wa Adamu,...*

<sup>154</sup> Jamani! Mliona? Nyota, vinara vya taa, taa. Vinamaanisha nini? Hii inamaanisha nini? Kwamba muda wa wakati tunaoishi ni usiku, mishumaa na miangaza na nyota zinamaanisha usiku. Nayu nyota hufanya nini? Huakisi nuru ya jua mpaka jua litakaporudi. Jina la Bwana libarikiwe! Naye mhudumu wa kweli wa Mungu haakisi tochi fulani, miti fulani ya kiberiti, kapi fulani likiwaka; yeye huakisi miale ya dhahabu ya Kristo kwa Kanisa, kwamba "Ni yeye yule, Naye yu hai, Naye ananawiri juu yangu." Amina! Hiyo ndiyo Nuru anayoakisi. Nyota huakisi nuru ya jua, mnaona, kwa hiyo tunaakisi Nuru ya Mwana wa Mungu. Tukifanya jambo lile lile alilofanya Yeye, tukitoa Nuru. Nuru ya aina gani? Nuru ya Injili kwa hao.

<sup>155</sup> Sasa hebu tumwangalie kidogo zaidi, tunapochukua sehemu iliyobaki ya kifungu hiki cha 13:

... *Na katikati (hiyo ni katikati) ya vile vinara vya  
dhahabu nikaona mtu mfano wa...Mwana wa Adamu,  
amevaa vazi lilofika miguuni, na amefungwa mshipi  
wa dhahabu matitini.*

<sup>156</sup> Sasa hili hapa thibitisho zaidi kwamba fundisho hili ni la kweli kuhusu hii kuwa ni siku ya Bwana. Hivi mlimwona? Yeye hakuwa kuhani wakati huu, wala hakuwa mfalme,

Yeye alikuwa ni hakimu. Angalieni, kuhani, kuhani mkuu, alipoingia madhabahuni ama alipoingia apate kuhudumu, kufanya ibada, alijifunga kiunoni. Kuufunga mshipi wake kiunoni kulimaanisha ya kwamba alikuwa akitumika; kamwe hakuufunga begani mwake. Lakini hapa anatoka, akitembea huku mshipi umefungiwa juu, amefunga mshipi begani Mwake; umefungiwa matitini, kifuani, kwa mshipi wa dhahabu, umefungiwa juu. Ni nini? Wakili, hakimu. Hakimu amejifunga mshipi begani mwake, umefungiwa hapa, sio chini kama kuhani. Mnaona, hiyo inaonyesha Yeye hakuwa katika ukuhani Wake sasa, Yohana alienda mpaka akaingia katika siku ya Bwana na kumwona akija kama hakimu.

<sup>157</sup> Mnaamini Yeye ni hakimu? Hebu tusome Yohana Mtakatifu 5:22, upesi sana, tutaona kama Yeye ni hakimu ama la. Yohana Mtakatifu 5:22:

*Tena Baba hahukumu mtu ye yote, bali amempa  
Mwana hukumu yote:*

<sup>158</sup> Hiyo ni kweli? Yeye ni hakimu, Hakimu Mkuu. Naye Yohana anaonyesha ya kwamba hakuwa katika siku za unabii Wake, kama nabii, wala Yeye hakwenda hata kwenye siku za ufalme Wake, bali alikuwa katika siku ya Bwana kama Hakimu. Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba kuhani akiwa na mshipi wake, mshipi wake kiunoni mwake ilimaanisha alikuwa katika huduma? Kila mtu anayesoma hayo Maagano, anajejua Agano la Kale, anajua hivyo. Wakati kuhani amefunga mshipi hapa, yuko katika huduma, yeye ni mtumishi. Bali aliufunga hapa juu, hakimu.

<sup>159</sup> Hebu tusome mbele kidogo:

*...mshipi wa dhahabu...ulikuwa...matitini...*

<sup>160</sup> Hiyo ni kweli, hapa *juu*, Yeye alikuwa ni Hakimu.

Sasa tutasoma utukufu wa Utu Wake wenye sehemu saba. Loo, jamani! Hili linanifanya nipige makelele kabla sijalifikia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Angalieni! Loo, hili ni jambo zuri sana. Hebu sikilizeni tu:

*Na kichwa Chake...*

<sup>161</sup> Sasa angalia, Yeye ni vitu saba, hapa anataja: kichwa Chake, nywele Zake, macho Yake, miguu Yake, sauti Yake... Vitu saba alivyotaja hapa, utukufu wa Yesu Kristo wenye sehemu saba. Hebu niusome:

*Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama  
sufu, nyeupe kama theluji;...macho yake...miali ya  
moto;*

*...miguu yake...shaba iliyosuguliwa sana, kana  
kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake...  
sauti ya maji mengi.*

*Na katika...Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume: na upanga mkali, wenyе makali kuwili ulitoka katika kinywa chake: na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake.*

<sup>162</sup> Ni ono la jinsi gani! Yeye aliona kitu gani hapa? Mwana wa Mungu aliyetukuzwa, na ishara. Sasa, hebu—hebu na tuwe tayari sasa.

<sup>163</sup> Loo, jamani, nilifikiri hiyo ilikuwa ni saa tatu, ni saa mbili tu. Sijaanza bado. Vema. Hilo ni jema. Sasa, samahani ndugu hawa wanaosimama, inanitia wasiwasi kuwaona wamesimama, mnaona, maana ninajua miguu yao inauma. Laiti ningalikuwa na njia yoyote ndugu, ya lolote ningaliweza kufanya, hakika ningelifanya. Sasa, ninawatakeni mpate hili sana. Na msimame muda kidogo na Mungu awajazi sana, ndilo ombi langu.

<sup>164</sup> Sasa—sasa angalieni, jambo la kwanza, sasa tunaona, Kichwa chake na nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu. Kichwa Chake na nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu. Sasa, haimaanishi ya kwamba alikuwa amezeeka, ndio uliosababisha hili. Hiyo siyo sababu yake. Hakuwa amezeeka kufanya jambo hili. Alikuwa... Ilikuwa ni kwa sababu ya ujuzi Wake na sifa na hekima Yake. Kwa sababu Yeye ni wa Milele, na Milele haiwezi kuzeeka. Mnaelewa?

<sup>165</sup> Hebu tufungue kwanza, nasi tuta—tatamwangalia hapa nje hivi, na tutaona kwamba Yeye ni nini. Sasa, hebu tufungue Danieli 7:9, kwa dakika moja tu, mtaona picha ile ile katika Danieli ambapo Yeye anakuja kama... hapa kwenye Mzee wa siku. Na karibu kila mtu, mwanafunzi wa Biblia, anajua hasa mahali tunapoelekea sasa hivi. Danieli 7, na kifungu cha 9; nitaanza kwenye cha 8:

*Nami nikaangalia sana pembe zake, na, tazama, pembe nyingine ikazuka...nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele—mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa: na, tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama...ya mwanadamu, na kinywa kilikuwa kikinena maneno makuu.*

Tena nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa,...

<sup>166</sup> Sasa sikilizeni. Sikilizeni kwa makini, sasa. Je, mwaweza kunisikia huko nyuma vizuri? Semeni, "Amina," kama mnaweza. Nilimwuliza mke wangu nyuma pale. Nafikiri maikrofoni hii hapa ni... hii inafanya kazi vizuri zaidi hapa, sivyo? Sasa, ninapiga makelele kwa nguvu sana, nadhani, katika hii.

<sup>167</sup> Vema, sasa Danieli 7:9:

*Tena nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye Mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama...sufu safi; (Mzee wa siku.) ...kiti chake*

*cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake kama moto uwakao.*

Nao mto kama wa moto—moto ukatoka ukapita mbele zake: na maelfu maelfu walimtumikia, na kumi... mara elfu kumi walismama mbele yake: na hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.

<sup>168</sup> “Nywele nyeupe!” Wote...mtu yeoyote anajua hao ni mahakimu wa zamani za kale. Kama mahakimu wa Kiingereza walikuwa wakivaa wigi nyeupe kama theluji. Ni wangapi wanakumbuka hilo? Mahakimu wa kale walivaa wigi nyeupe kwa sababu walikuwa...Naye huyu hapa, kuonyesha tena kwamba Yohana yuko katika siku ya Bwana, alimwona kama hakimu. Amina! Sio kama kuhani, sio kama mfalme, sio kama nabii, bali kama hakimu. Baba (Ni Yohana Mtakatifu 5:22) alimkabidhi hukumu yote. Naye ni hakimu sasa, amekuja kuyahukumu mataifa. Loo kwa siku hiyo wakati utamwona namna hiyo! Nywele Zake zilikuwa nyeupe kama theluji, Danieli alimwona akija kwa yule Mzee wa siku. Mtazame akichanganya hizi mbili pamoja. Vema:

...na hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.

Na nikaona basi kwa sababu...Tena nikaona wakati huo kwa sababu ya sauti ya ma—maneno makubwa ambayo pembe... (Hapanana, nimefungua mahali pengine, sivyo?)

<sup>169</sup> Danieli 7:9, naam, haya basi:

...na magurudumu yake...

Nao mto kama moto ukatoka ukapita...ukatoka... mbele zake: ndipo makumi ya maelfu wakaja na wakamtumikia,...

Basi nikatazama wakati huo kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyoyasema ile pembe: nilitazama hata mnyama yule akaauawa, mwili wake ukaharibiwa, akatolewa a—ateketezwe kwa moto. (Uhm!)

Na kwa habari za wale wanyama wengine, wote walinyang'anywa mamlaka yao: (hiyo ni kwamba mamlaka yote ya Mataifa na falme zao zitaanguka) walakini maisha yao yalidumishwa kwa wakati na majira.

Ndipo nikaona katika njozi ya usiku, na, tazama, mmoja aliye mfano wa Mwana wa Adamu akaja katika...mawingu ya mbinguni,... (Tulimwona akija namna gani asubuhi ya leo, katika kifungu cha 3? Akija katika mawingu ya mbinguni, Mwana wa Adamu.) ... aliye mfano wa Mwana wa Adamu akija katika

*mawingu ya mbinguni, akamkaribia huyo Mzee wa siku, wakamleta karibu naye.*

*Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, na watu wa kacula zote, na mataifa yote, . . . lugha zote, wamtumikie; haya mamlaka ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake utaninii . . . ufalme wake ni ufalme usioweza kuanguka.*

<sup>170</sup> Akaja kwa Mzee wa siku ambaye nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu. Naye Yohana akageuka akaona mmoja kama Mwana wa Adamu amesimama katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu, akiwa na nywele nyeupe kama thelaji, Hakimu! Hajafungwa kiunoni, lakini amejifunga matitini, juu hapa, hakimu! Akiwa na mshipi wa hakimu juu ya bega Lake, alisimama na mshipi wa dhahabu, safi, mtakatifu, uliosuguliwa sana, ambao ulishikilia haki Yake. Kifuniko Chake! Alifunikwa mpaka miguuni. Angalieni dhihirisho la utu na utukufu Wake wenye sehemu saba.

<sup>171</sup> Sasa, ninaamini, kifungu cha 14:

*Nywele zake . . . kichwa Chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, nyeupe kama thelaji; na macho yake . . . miali ya moto;*

<sup>172</sup> Kichwa, nywele; “macho yalikuwa kama miali ya moto.” Wazia hilo! Hayo macho ambayo wakati mmoja yalizima kwa machozi ya kibinadamu, sasa yamekuwa miali ya moto. Katika hasira anasimama kama hakimu mwenye hasira. Kwa nini ukamkataa? Loo, ewe mwenye dhambi, wazia hili! Wazia hilo, ewe mfuasi vuguvugu wa kanisa! Liwazie, ewe Mkatoliki, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mpentekoste! Liwazie hilo, ewe Mkatoliki! Ilimbidi bikira Mariamu wenu kwenda hadi pentekoste na kumpokea Roho Mtakatifu, na kuyumbayumba na kufanya kama mwanamke mlevi. Ilimbidi mama ya Kristo mwenyewe kumpata huyo kabla hajaruhuswa kuingia Mbinguni. Ninyi wanawake mtafika huko vipi kwa chochote pungufu ya hicho? Wazieni hilo, wanaume, kila mmoja wenu!

<sup>173</sup> Nywele Zake, na macho yake yalizima wakati mmoja kwa machozi ya kibinadamu, hata hivyo ninawatakeni muone kitu fulani kuhusu macho hayo. Wakati alipokuwa angali duniani, yalizima kwa machozi kama mwanadamu, kwa kuwa alilia kwenye kaburi la Lazaro. Kweli! Alijaa huruma; uwanaadamu Wake. Yeye alivikwa, alikuwa ni Mungu alihevikwa uwanaadamu, apate kuondoa dhambi. Lakini hata hivyo nyuma ya uwanaadamu huo, Yeye alikuwa na kitu fulani nyuma Yake ambacho kingeangalia moja kwa moja katika moyo wa mwanadamu na kujua yote kumhusu. Kwa nini? Kulikuwa na kitu fulani nyuma Yake, hata hivyo alivikwa mwili unaopatikana na mauti.

<sup>174</sup> Lakini hawakujuu alikuwa nani. “Kama hamwamini,” Yeye alisema, “ya kwamba Mimi ndiye, mtakufa katika dhambi

zenu.” Hiyo ni kweli. “Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi; bali kama nikizifanya kazi za Baba Yangu, basi aminini kazi hizo kama hamwezi kuniamini Mimi.” Loo, jinsi alivyajaribu kuwapelekea Ujumbe, ufunuo. Angeweza kuangalia moja kwa moja katika moyo wa mwanadamu, ajue yote kumhusu. Jinsi ninavyoliwazia hilo: Macho hayo ambayo wakati mmoja yalichungulia juu ya milima, yakaangalia kwenye uso wa mateso, na yangeweza kulia kama mwanadamu, bali hata hivyo yangeichukua Roho ya Mungu nyuma ya ono hilo la kibinadamu pale na kuona mambo yote; mambo yaliyokuwako, hayo mambo ambayo yalikuwako—yalikuwako, na mambo yatakayokuja. Akatabiri mwisho tangu mwanzo, hiyo ni kwa sababu Mungu alikuwa nyuma ya macho hayo ya kibinadamu. Acha Mungu aje maishani mwako na kuchukua mamlaka juu yako, Naye atakuonyesha mambo yajayo. Kwa kuwa si wewe tena, ni Roho Mtakatifu maishani mwako huko nyuma akiangalia kupitia kwa macho hayo ya kibinadamu apate kuyaona mambo hayo.

<sup>175</sup> Loo, utukufu kwa Mungu! “Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili, na wana na binti zenu watatabiri, vijana wenu wataona maono, wazee wenu wataota ndoto.” Haleluya! Wakati mwingine inambidi kukuweka usingizini apate kutazama kupitia kwako, bali hakika atakuonyesha mara nyingi. “Vijana wenu wataona maono, wazee wenu wataota ndoto; juu ya wajakazi Wangu wa kiume na wa kike nitaimwaga Roho Yangu.” Sio, “Juu ya mashemasi Wangu na wachungaji, na juu ya nanii Wangu . . .” “Juu ya ye yeyote atakaye, juu ya wote wenye mwili, nitaimwaga Roho Yangu.” Mnashangaa ni kwa nini ninasema hayo kwa sauti kuu, bali linakuja katika nyakati hizi za kanisa.

<sup>176</sup> Loo, Huyo hapo, macho hayo. Na, kumbukeni, siku moja, macho hayo yaliyokuwa yamezima kwa machozi, macho hayo yatasimama hukumuni. Sasa ni kama miale ya moto ikienda mbio huku na huku duniani kote, wala hakuna kitu kinachotendeka bila Yeye kujua. Loo, jamani, imerekodiwa. Yakienda mbio huku na huku duniani yakiangalia kila msogeo, yakinambua kila wazo, akijua kila kitu unachofanya, makusudi ya moyo, kile unachokusudia kufanya. Yeye anajua yote kuhusu jambo hilo. Yeye anajua kama unampenda. Anajua kama nia yako ni sawa, kumtumikia. Anajua yote kuhusu hilo. Basi itakuwaje wakati utakaposimama siku hiyo wakati kila dhambi imewekwa wazi mbele Zake, Naye amesimama pale kwenye Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi?

<sup>177</sup> Mungu, niokoe na mahali hapo! Sitaki kuona hayo. Wakati Mungu mwenye hasira atakapoenda pale huku moto unamulika kutoka machoni Mwake, kwa haki, wigii nyeupe juu ya kichwa Chake namna hiyo, nayo macho Yake yakimulika kwa moto unaojua kila wazo la moyo wako, na kila kitu ulichokusudia

kufanya. Nifiche katika Mwamba wa Miaka uliopasuliwa kwa ajili yangu! Yule mzee alizoea kuimba, "Wakati ulimwengu huu wote unawaka moto, simama karibu nami. Simama karibu nami, na kifua Chako kiwe foronya yangu. Nifiche kwenye Mwamba wa Miaka." Mungu, siitaki hukumu Yako. Sitaki ninii Yako... Kile ninachotaka ni rehema Yako, Bwana. Nipe rehema Yako, sio haki Yako ya Haki. Nipe tu rehema Yako. Sio torati Zako, sio ninii yoyote... Nipe tu rehema, Bwana, hiyo tu ndiyo niwezayo kuomba. Sina cha mkononi (mimi si mwema, sifai kitu), ninashikilia tu msalabani Pako. Bwana, hilo tu ndilo nijualo: Mtu mmoja alikuja kupachukua mahali pangu.

<sup>178</sup> Angalieni utu Wake wenyе sifa saba sasa, nanyi mtaona aliyofanya.

*Kichwa chake... kilikuwa cheupe kama theluji; kama sufu, nywele nyeupe; na macho yake kama... (hebu tuone)... Kichwa chake... zilikuwa nyeupe kama... theluji; na macho yake... miale ya moto;*

*Na miguu yake kama... shaba iliyosuguliwa sana, kama kwamba imechomwa katika tanuru;*

<sup>179</sup> Angalieni sasa. Ndiyo kwanza tuone mahali alipofunikwa, mwajua. Sasa angalieni. Kichwa Chake, macho Yake, sasa Yeye anashuka kwenye miguu Yake kama shaba. Angalia mlinganisho wa sanamu hiyo hapo ya Yesu ambayo Yahana aliiona, na ile Danieli aliyoiona ya falme za ulimwengu, kichwa cha dhahabu na kadhalika.

<sup>180</sup> Angalia kile hii ilichokuwa hapa, ikisimama pale, shaba. Shaba inanena juu ya nini? Shaba inanena juu ya hukumu, hukumu ya Kiungu. Inaonyesha ya kwamba kusudi Lake lote ni kuja hapa duniani kama Mungu, afanyike mwili, Naye akafa kwa ajili yetu na kuchukua hukumu ya Mungu, hukumu ya Kiungu, naye amepokea Ufalme ambao ni shaba, na mgumu, wala hauwezi kutikiswa. Hakuna kitu kilicho kigumu kuliko shaba, wala hawajapata kitu ambacho ungekichanganya nayo.

<sup>181</sup> Hukumu! Shaba hunena juu ya hukumu ya Kiungu iliyopitishwa. Angalia yule nyoka wa shaba nyikani. Huyo nyoka wa shaba aliwakilisha nini? Huyo nyoka aliwakilisha dhambi; lakini, kwa kuwa ni shaba, ni hukumu iliyopitishwa tayari juu ya dhambi.

<sup>182</sup> Sasa, angalia pia siku za Eliya, walipokuwa wamemkataa Eliya kama nabii, ule uzi mdogo, ule wakati wa kale wa kanisa. Moja ya siku hizi nitaleta na kuwaonyesha ya kwamba Israeli ilikuwa na nyakati saba za kanisa, pia, nazo zilifanana kabisa na hizi. Na katika wakati wao wa kanisa, katika siku za Eliya, walimkataa na kuna miaka mitatu na miezi sita hapo hakukuwako na mvua. Naye huyo nabii wa kale akasema kwamba "mbingu zilionekana kama shaba," hukumu ya Kiungu

juu ya mataifa kwa ajili ya kumkataa Mungu na kumsikiliza Yezebeli.

<sup>183</sup> Shaba pia inawakilisha hukumu ya Kiungu madhababuni ambapo sadaka iliuawa, madhababu ya shaba. Kuuawa... Misingi yenyewe ilikuwa ni ya shaba, hukumu, Yeye alikanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu na kuichukua hukumu yetu juu ya nafsi Yake. Fungueni Ufunuo 19:15, kwa dakika moja tu, hebu tuone kile alichofanya. Ufunuo 19:15, hebu tusome tu kwa dakika moja kama ninaweza kupapata. Naam, hebu tuanzie kwenye...hebu tuone, yapata kifungu cha 12:

*Na macho yake...miale ya moto, na juu ya kichwa chake kilemba, vilemba vingi; naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila...mwenyewe.*

*Naye amevikwa vazi lililochovyywa katika damu: na jina lake liliitwa, Neno la Mungu. (Sasa, kumbukeni, Jina Lake halikuwa ni Neno la Mungu, aliiitwa Jina Lake hivyo. Mnaona?)...jina lake aliiitwa, Neno la Mungu.*

*Na majeshi...ya mbinguni...majeshi yaliyokuwa mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe, na kuvikwa kitani nzuri nyeupe, safi.*

*Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige taifa kwa huo: naye atawachunga kwa fimbo ya chuma: naye atakanyaga... (Hicho ni nini?)...kanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi.*

<sup>184</sup> Yeye alifanya nini? Hasira ya Mungu ilikuwa juu yetu kwa ajili ya kuwa wenye dhambi. Hiyo ni kweli? Hakuna mtu angaliweza kujiokoa. Hakuna kitu tungaliweza kufanya, sisi sote “Tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo.” Naye alifanya nini? Alikuja duniani, Haleluya, na kukanyaga shinikizo la mvinyo! Hasira yote ya Mwenyezi Mungu ilimwagwa juu Yake. “Umestahili, Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, kwa kuwa ulichinjwa.” Akichukua dhambi za ulimwengu juu ya nafsi Yake, Naye akaichukua dhambi yetu, hata Mungu akamwaga ghadhabu ya hasira Yake juu Yake. “Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa uovu wetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Hakuna mtu aliyepata kufa kama Mtu huyo! Yeye aliteseka hata damu na maji vikatengana mwilini Mwake. Na matone ya damu yakatoka usoni Mwake kabla ya kufa Kwake.

*...shinikizo la mvinyo ya...hasira...ya ghadhabu ya hasira...ya Mungu Mwenyezi.*

<sup>185</sup> Siku moja hiyo miguu ya shaba ya haki (Utukufu!), wakati atakapokuja kama hakimu, Yeye atamkanyaga mpinga-Kristo,

pamoja na adui Wake wote. Haleluya! Atatembea duniani akiwa na fimbo ya chuma mkononi Mwake. Amina! Loo, tubu, ewe rafiki mpendwa, wakati ukiwa na nafasi ya kutubu. Jaribu, iweke kando na kuwazia ni hadithi ndogo tu ambayo haitatukia. Itatukia! “Isingetukia kamwe kwango.” Itatukia kwako!

<sup>186</sup> Miguu ya shaba, anawakanyaga adui Zake. Kwa sababu aliteseka na kukanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu kuzilipia dhambi zetu. Na kisha sisi, maskini wadudu wenyе hatia, wenyе mashaka kama sisi, tunainua pua yetu juu na kusoma namna fulani ya vitabu vya kikafiri na kujaribu kuwazia “hakuna Mungu,” na kusema “hakuna kitu kama *hiki*, wala hukumu haiwezi kuja.” Yeye ataichukua miguu hiyo ya shaba na kumponda adui Wake. Atamkanyaga mpinga-Kristo. Atayachukua makanisa hayo yenye ukengeufu na kuyatupilia mbali kwenye Umilele huko ng’ambo, mahali fulani katika moto ulao ambako atachomwa na kuangamizwa. Naye atatawala duniani, Yeye pamoja na Kanisa Lake milele. Utukufu!

<sup>187</sup> “Kichwa, cheupe kama sufu,” haki, ujuzi, ufasaha, utoshelevu, hekima. Mzee, mweupe, inanena kuhusu hekima, mzee. Anajua analofanya. Yeye ni—Yeye ni Chemchemi ya hekima. Yeye ni Chemchemi ya ujuzi. Yeye ni Chemchemi ya kila kitu kilicho chema, kwa hiyo amewakilishwa katika huyu aliye kama Mwana wa Adamu, aliyeava nyewe hizi nyeupe zinazoning’inia chini. Danieli alimwona mamia mengi ya miaka, miaka mia saba, na kusema, “Yeye alikuwa Mzee wa siku. Na mmoja kama Mwana wa Adamu akija katika nguvu na akaungana na huyu Mzee wa siku, ndipo hukumu ikawekwa.”

<sup>188</sup> Sasa ninataka tu kuwaauliza jambo fulani. Ninasema nanyi enyi kanisa vuguvugu. Wanawali kumi walienda kumlaki Bwana, watano wao walikuwa na busara, watano wapumbavu; kama tulivyouchukua asubuhi ya leo, mti ule uliopandikizwa. Sasa, kumbukeni, wakati walipokuwa wakienda kumlaki Mungu... Sasa angalieni, Biblia ilisema, “Vitabu vilifunuliwa.” Danieli 7:9, “Vitabu vilifunuliwa.” Hicho ni kitabu cha mwenye dhambi. “Na kitabu kingine kikafunguliwa.” Ni nani aliyejukua pamoja na Yeye? Lile Kanisa lilitotoka kwenye Unyakuo. Loo! “Makumi ya maelfu mara maelfu mara maelfu ya maelfu waliambatana na Yeye na kumhudumia,” Mke Wake, Bibi-arusi. Loo, utukufu! Mke wake aliambatana Naye, lile Kanisa.

<sup>189</sup> Hukumu iliwekwa, na vitabu vikafunguliwa. Na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni mwanamwali aliyelala, na kila mtu alihukumiwa kutoka kwenye kitabu hicho. Utatakiwa kutoa sababu ni kwa nini hukuamini, ndipo nini basi? Unajua vema zaidi sasa, unajua vema zaidi. Huenda hukujua Hilo hapo awali, bali unajua sasa. Unaona? Ambapo kama huyu mwenye haki ataokoka kwa shida, huyo mwenye dhambi na asiye mtauwa ataonekana wapi? Yule anayekataa, anajua vema zaidi

halafu analikataa. Wataonekana wapi? Miguu Yake kama shaba, hukumu ya Kiungu.

<sup>190</sup> Sasa, hebu tuone, karibuni tutaninii . . . chini mwishoni mwa ukurasa sasa:

. . . nywele kama sufu, . . . na macho yake yalikuwa . . .  
miale ya moto;

*Na miguu yake kama—miguu yake kama . . . shaba, . . . imesafishwa katika tanuru; na sauti yake . . . sauti ya maji mengi.*

<sup>191</sup> “Sauti ya maji mengi.” Maji yanawakilisha nini? Kama unataka kuandika, fungua Ufunuo 17:15, na utakuta kwamba Biblia ilisema, “Maji uliyoona yalikuwa ni tabaka, na makutano, na jamaa, na lugha.”

Vema, “Sauti.” Ni jambo la kutisha jinsi gani kwa nafsi inayoelea kwenye bahari ya maisha! Hakuna nahodha wa kumwongoza, ameachiliwa, anachukuliwa na mkondo wa maji, kusikia mgurumo wa maporomoko makubwa ya maji, maporomoko. Ni jambo la kutisha jinsi gani kwa nafsi inayoelea. “Sauti ya maji mengi.” Sauti Yake ni nini? Ni hukumu; sauti ya wahudumu, kupidia kwa Roho Mtakatifu, waliopaza sauti kwa watu katika kila wakati, wakisimama pale. Sauti ya maji mengi ilipaza sauti, tabaka na makutano. Sauti ya hizo nyota saba mkononi Mwake, kwa kila wakati wa kanisa, zikihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, ubatizo katika Jina la Yesu, kunena kwa lugha, uweza wa Mungu, ufuluo wa Kristo, Kuja Mara ya Pili, hukumu ya Kiungu. Sauti ya maji mengi ilitoka kwa huyu aliyefanana na Mwana wa Adamu, maji mengi.

<sup>192</sup> Jinsi itakavyokuwa kujua ya kwamba uliketi mkutanoni na kusikia ya kwamba unapaswa kujiweka sawa na Mungu na kumpokea Roho Mtakatifu, nayo nafsi inayoelea kusikia sauti hiyo ikinena kwenye mkutano ulimoketi, na kusikia hukumu za Mungu zikihubiriwa, na kulikataa. Lile poromoko kuu liko tu hapo chini yako, yale maporomoko makuu yatakayokupeleka kwenye maangamizi yako ya Milele.

<sup>193</sup> Sauti ya maji mengi, utu Wake wa nne. Sauti ya maji mengi. Utafanyaje hilo wakati limeandikwa Utukufuni, wakati sauti usiku wa leo imerekodiwa? Sauti yako inarekodiwa. Mawazo yako yanarekodiwa. “Jinsi mtu awazavyo moyoni mwake, ndivyo alivyo.” Angalia, sauti yako inasikika zaidi Mbinguni kuliko ninii yako . . . namaanisha, mawazo yako yanasisikika zaidi Mbinguni kuliko sauti yako inavyosikika duniani. Hakika, yanasisikika. Mungu anajua mawazo na makusudi ya moyo, Yeye anajua yote kuyahuusu.

<sup>194</sup> Yeye alimwambia Mfarisayo, “Enyi wanafiki, mnawezaje kunena mema, wakati kinywa cha mtu hunena yaujazayo moyo wake? Kuniita Mimi, ‘Bwana, mwema,’ wakati najua, ninawenza

kuangalia moja kwa moja ndani yako na kuona ya kwamba wewe ni mnafiki. Humaanishi hilo."

<sup>195</sup> Loo, hiyo itakuwaje kwenye siku hiyo wakati sauti hiyo ya ngurumo kutoka kwenye maji mengi, nyakati nyangi za kanisa zikiumbika?

<sup>196</sup> Sasa nataka kuwaulizeni jambo jingine. Hebu niwaambie jambo fulani ninyi watu mlioookoka, hebu niwaambieni jambo hili.

<sup>197</sup> Sasa, ewe nafsi inayoelea, maskini ewe mzururaji unayeelea juu ya lile poromoko kubwa huko, kuwa mwangalifu. Litakuwa ni jambo la kutisha sana kwako utakapoju ya kwamba hakuna wokovu kwako basi. Huwezi kuokolewa wakati huo, unajua maangamizi yako yako moja kwa moja mbele zako. Wakati ukijua katika dakika chache utaisikia Sauti hiyo ikisema, "Ondokeni Kwangu, enyi watenda maovu, mwingie kwenye moto wa milele uliofanywa tayari kwa ajili ya ibilisi na malaika zake." Utajua wakati utakapoyasikia maporomoko hayo makubwa yakingurumisha sauti hizo za mikutano hiyo, wakati ukiondoka kutoka kwenye huu. Loo, ni jambo la kusikitisha jinsi gani, ni jinamizi ya jinsi gani! Msiache hilo liwapate, enyi watu. Tubuni, iweni sawa na Mungu sasa, wakati mnapoweza kuwa sawa.

<sup>198</sup> Sasa nataka kuwaulizeni jambo lingine. Ni kitu gani kilicho kitamu zaidi kwa mtu aliyetia nanga, amelala huko chini ya mti usiokauka, kusikia kijito cha kiwimbi-wimbi? Loo! Hilo ni Kanisa limeketi katika mahali pa mbinguni huku Sauti ya Mungu ikilia vizuri kama mawimbi na kuwazungumzia basi. Mnaona ni kitu gani? Ni hukumu kwa mwenye dhambi, na baraka kwa aliyeokoka. Mtu ambaye ametia nanga salama mashua yake juu ya Mwamba Kristo Yesu, naye anakaa tu na kusikiliza, jinsi anavyoweza kustarehe! Kuingia katika raha hiyo.

<sup>199</sup> Jinsi ninavyopenda kufika mahali ambapo maji yanatiririka. Kama tukipata kwenda kuvua samaki ama chochote kile, mara nyangi mimi hujaribu kupata mahali ambapo maji yana mawimbi-wimbi, maana hukufanya tu ustarehe. Unayasikia yakizungumza tu usiku kucha. Loo, jamani!

<sup>200</sup> Si ni vizuri sana wakati unapoweza kweli kuitia nanga nafsi yako katika Kristo, kufikia mahali ambapo unaweza kutulia mbele Zake? Na kusikia Sauti Yake ikisema nawe, "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye. Mimi ndimi Bwana nikupaye Uzima wa Milele. Ninakupenda. Nilikujua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Niliandika jina lako kwenye Kitabu, wewe ni Wangi. Usiogope, ni Mimi. Usiogope, niko pamoja nawe." Ndipo ninaimba:

Nimetia nanga nafsi yangu katika mahali pa  
raha,  
Sitaabiri bahari zenyen tufani tena;

Huenda tufani ikakipiga kilindi cha bahari  
yenye dhoruba;  
Lakini katika Yesu mimi ni salama milele.

<sup>201</sup> Kumbukeni, Sauti ile ile inayokuzungumzia kwa utamu, itamhukumu mwenye dhambi. Gharika ile ile iliyomwokoa Nuhu, ilimwangamiza mwenye dhambi. Mnaona ninalomaanisha? Sauti ya maji mengi.

<sup>202</sup> Angalieni sasa, “Nywele kama sufu, na macho kama miali ya moto, miguu kama shaba, na sauti kama ya maji mengi.”

*Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume: . . .*

<sup>203</sup> “Nyota saba.” Sasa hebu tuchukue kifungu cha 20 papa hapa:

*Basi siri ya zile nyota saba ulizoona katika mkono wangu wa kuume, na vile vinara vya taa saba vya dhahabu. Zile nyota saba ni malaika saba (ama wajumbe saba, wahudumu saba) wa yale makanisa saba: na vinara vya taa saba ulivyoviona ni yale makanisa saba.*

<sup>204</sup> Yeye anamfasiria ili kuwe na hakika kwamba hapatakuwa na kosa lolote. Malaika mmoja kwa kila wakati wa kanisa. Loo, hilo litakuwa ni zuri sana, juma hili, tutakaporudi huko katika historia na kuwachukua malaika hao na kuona huduma yenewe waliyokuwa nayo. Walikuwa na huduma ile ile. Ile ile hasa kote katika wakati katika maskini Kanisa hilo.

<sup>205</sup> Wakati fulani uliopita, mtu fulani alisema, “Mnajua, kanisa Katoliki, kuna msemo mzuri, ya kwamba, ‘Ndilo kanisa halisi kwa sababu limesimama kote katika nyakati.’”

<sup>206</sup> Nikasema, “Hiyo si siri, wakati lilipokuwa na serikali yote na kila kitu nyuma yake, na jinsi lilivyosimama na kuistahimili dhoruba. Lakini siri kwangu ni vile lile kanisa dogo, la uchache lingaliweza kamwe custahimili dhoruba, ambapo walikatwa kwa misumeno, wakatupiwa simba, na kuwekwa kwenye kitanda cha kuwanyoshea, na kuliwa, na kuchomwa, na kwa simba . . . na kuuawa na kadhalika, na jinsi walivyoponea hayo.” Inaonyesha ya kwamba mkono wa Mungu ulikuwa pamoja nao. Hivyo tu. Na hata wa leo Nuru yake ingali inawaka. Amina! Naam, bwana!

<sup>207</sup> Sasa, “Zile nyota saba zilizokuwa katika mkono Wangu wa kuume.” Yeye alikuwa na nyota saba katika mkono Wake wa kuume, ambazo zinamaanisha wahudumu saba wa nyakati saba. Loo, ni—ni zuri. Jinsi tunavyorudi nyuma na kumpata m—mhudumu aliyeleta Ujumbe kwa kanisa la Efeso. Na mhudumu aliyeleta Ujumbe na kuushikilia mpaka kufa, moja kwa moja hata kwenye kanisa la Smirna, na kwa kanisa la Pergamo, Thiatira, na kuendelea kote katika wakati, hata kufikia kwenye

wakati huu sasa. Wahudumu waliendumisha na kuileta Nuru, na kuishikilia kama ile ya asili hapo mwanzo, na kuileta Nuru kupitia kwake.

<sup>208</sup> “Alizishika katika mkono Wake wa kuume.” Wazia! Mkono wa kuume haumaanishi hasa kama Kristo kuketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Haimaanishi kwamba Mungu ana mkono wa kuume, kwa sababu Mungu ni Roho. Lakini Kristo alikuwa ni mkono wa kuume wa nguvu. Mtu wako wa mkono wa kuume, yule jamaa—jamaa anayesimama karibu nawe, aliye karibu zaidi na wewe.

<sup>209</sup> Basi, kumbukeni, zile nyota saba zilikuwa kwenye mkono Wake wa kuume. Wazieni tu, walikuwa waupate umeme wao, Nuru yao kutoka Kwake. Walikuwa chini ya mamlaka Yake kabisa, katika mkono Wake wa kuume. Loo! Kila mtumishi wa kweli wa Mungu ni vile vile. Wameshikwa katika... Ni nani awezaye kuwadhuru? Ni nani awezaye kuwadhuru? Kama vile mmoja wa hao malaika alivyosema kwa sauti kuu huko nyuma katika mwanzo. Kumbukeni *malaika* maana yake ni “mjumbe.” Tutaingia katika mambo hayo yenyé kilindi baadaye wiki hii. *Malaika* linamaanisha “mjumbe.” Naye alisema, “Ni kitu gani kinachowenza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo? Ugonjwa waweza? Hatari inaweza? Uchi unaweza? Upanga unaweza? Mauti yanaweza? Nimeshawishika” kasema Paulo, “ya kwamba hakuna kitu kinachowenza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo,” kwa kuwa tumejisalimisha kabisa katika mkono Wake wa kuume.

<sup>210</sup> Mtu fulani akisema, “Mtakatifu anayejibingirisha! Mtakatifu anayejibingirisha!” Hiyo haiwasumbui hata kidogo. “Wewe ni mlokole wa kidini!” Hata hawalisikii. Wamejitolea kabisa na wanavuta Maisha yao kutoka kwa mkono Wake wa kuume wa nguvu, wakiuakisi Mwangaza Wake katika upole, na wema, na upole, na subira; ishara, na maajabu, na miujiza. Acha ulimwengu uuite “uchawi,” chochote wanachotaka, haitufanyi tofauti yoyote, kwa sababu tunajua tumejitolea na katika mkono Wake wa kuume. Hilo si ni zuri sana? Jamani!

<sup>211</sup> Sasa hebu tuharakishe, maana hatutaki kuwachosha. “Katika mkono Wake wa kuume, nyota saba.”

<sup>212</sup> Sasa uwakilishi wa saba na wa mwisho wa utu Wake:

...na upanga mkali wenyé makali kuwili, unatoka  
katika kinywa chake:...

Nilimaanisha, hiyo ni ya sita.

...na upanga mkali wenyé makali kuwili, unatoka  
katika kinywa chake:...

<sup>213</sup> Sasa, Sauti ya maji mengi, na kutoka kinywani Mwake... Katika mkono Wake wa kuume alikuwa na zile nyota.

*...na upanga mkali wenyе makali kuwili, unatoka katika kinywa chake:...*

<sup>214</sup> Sasa je, mnajua upanga mkali wenyе makali kuwili wa Biblia ni nini? Hebu tulishike tu kusudi mpate kujua. Fungueni Waebrania 4:2, kurudi tu nyuma ukurasa mmoja tu ama mbili mtalipata, mnaona. Waebrania iko tu nyuma ya Ufunuo hapa; Yuda, halafu Waebrania. Sasa, lipateni kwa makini sasa. Ama... Waebrania, mlango wa 4 wa Waebrania, haya basi. Vema, Waebrania mlango wa 4 na kifungu cha 12:

*Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu zaidi, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kugawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*

<sup>215</sup> Halafu wanakuita “msoma akili.” Ni Neno la Mungu lilodhihirishwa katika Kanisa Lake! Lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili. Aisee, ndiyo kwanza niwazie jambo lingine hapo. Sijui kama niliandika Andi... Fungueni Ufunuo 19, kwa dakika moja tu. Hebu tulipate hili tena, nafikiri hiyo ni kweli. Mimi labda... Ufunuo 19, yapata 11:

*Kisha nikazona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe;... (Hapa inakuja nyeupe tena, hukumu.) ...na yeye aliyempanda, aitwaye Mwaminifu na Wa-Kweli, naye kwa kweli... ahukumu na kufanya vita. (Mnajua huyo alikuwa ni nani, sivyo? Vema.)*

*Na macho yake yalikuwa...miali ya moto,... (Yeye alikuwa ni Nani?)...na juu ya kichwa chake kulikuwa...vilemba;... (Aa-loo. Tayari ameingia katika ufalme sasa.) ...naye ana...naye—naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila...mwenyewe.*

*Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu: na jina lake aitwa Neno la Mungu.*

<sup>216</sup> Ni kitu gani kilichotoka kinywani Mwake? Ni kitu gani kilitoka? Mpanda farasi mweupe. Nao Ufunuo, pia, 7, wakati... Ninaamini ni 8. Wakati yule farasi mweupe...la, ni 6. Wakati mpanda farasi mweupe alipotoka, Yeye alipewa u—uta, kushinda na apate kushinda.

<sup>217</sup> Nao upanga ukatoka kinywani Mwake. Yeye alikuwa ni nani? Yule mpanda farasi mweupe wa Ufunuo. Angalieni huo upanga. “Upanga mkali ukatao kuwili unatoka kinywani Mwake,” Neno. Na, hatimaye, kwa Upanga Wake, utakapodhihirishwa kwa wana wote wa Mungu, Yeye atakanyaga-kanyaga kila taifa kwa Upanga Wake, kwa upanga huu mkali. Angalieni hapa lililotukia, tunapolipata:

*Naye...mkono wake wa kuume...na upanga mkali wenye makali kuwili ukatoka katika kinywa chake: na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake.*

<sup>218</sup> “Upanga mkali ukatao kuwili.” Ni kitu gani kilikuwa kikitoka kinywani mwa mtu huyu? Neno la Mungu. Ni upanga mkali ukatao kuwili. Ulikuwa ukifanya nini? Ukiyatambua mawazo ya moyo, makusudi; unaingia hata ndani kuliko nyama, mwili, seli za damu, unaingia kwenye mfupa, chini kwenye mafuta ya mfupa, mpaka mbele ya hayo, hata kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Hivyo ndivyo Neno la Mungu linavyofanya.

<sup>219</sup> “Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Na sasa Neno amefanyika mwili katika Kanisa Lake, akikaa mionganoni mwetu. Malaika Wake mkononi Mwake, wakihudumu. Mungu analitegemea Kanisa Lake. Mungu anatutegemea sisi wa wakati huu kuileta Nuru hii ya Injili kwa ulimwengu wa mapokeo unaokufa, uliolemewa na ukafiri. Mungu anaweka mzigo huo juu yangu mimi na wewe. Ole wetu kama kafiri akifa bila kujua. Loo, walibeba kusoma, kuandika, na hisabati, na vijitabu vidogo vya kidini, nao hawajapata kitu ila kundi la wabadilisha dini. Ninamaanisha Injili! Injili si Neno pekee. Paulo alisema hivyo. Paulo alisema, “Injili haikuja kwetu kwa Neno pekee, bali hilo Neno likidhihirishwa.” Wakati Neno, kwa Roho Mtakatifu, ni... Neno limepandwa ndani ya moyo ulio na Roho Mtakatifu na linazaa kile Neno linachosema lingezaa. Nalo Neno linaweza kuyatambua mawazo ya moyo! Utukufu! Loo, jamani! Loo! Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo, Neno hufanya hivyo.

<sup>220</sup> Unatoka kinywani Mwake, upanga mkali wenye kukata kuwili, unawaamsha makafiri. Jambo fulani halina budi kutukia moja ya siku hizi. Naam! Neno la Mungu, Jina Lake liliwu ni Neno la Mungu, Neno lilodhihirishwa. Angalieni, Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote,” Marko 16, salamu Zake za mwisho kwa kanisa kabla hajarudi kujifunua Mwenyewe katika wakati wa kanisa. Yeye aliliagiza Kanisa, “Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Nini? Kuihubiri Injili. Marko 16, “Mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Hilo ni nini? Kwa maneno mengine, “mkazionyeshe nguvu za Roho Mtakatifu,” ilibidi iwe.

<sup>221</sup> Sasa angalia, “kwa kila...” Sio tu kulifundisha Neno; kamwe hakusema, “Enendeni mkalifundishe Neno.” Alisema, “Enendeni mkaihubiri Injili.” Sio kulifundisha Neno, kuihubiri Injili, “Na ishara hizi zitafuatana na hao wanaoiamini Injili hii; katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, wakishika nyoka ama kunywa kitu cha kufisha hakitawadhuru kamwe; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.”

<sup>222</sup> “Nao wakaenda,” kasema Maandiko, “wakihubiri kila mahali; Bwana akifanya kazi pamoja nao, akilithibitisha Neno kwa ishara zilizowafuata.” Hiyo ndiyo Injili, Injili katika wonyesho.

<sup>223</sup> Ishara hizi zitafuatana na wangapi? Hata mwisho wa ulimwengu, kwa kila wakati. Hao hapo maskini wale wachache wakishuka, wakiishikilia ile Nuru. Si ajabu Yesu alisema, “Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme.” Lile kundi dogo; daima ni wachache, sio wengi.

<sup>224</sup> Vema, sasa nukuu moja zaidi. Nasi tulichukua cha 20, kwa hiyo sasa hebu tuone hapa kwenye kifungu hiki hapa. Sasa cha 16:

*Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume: . . .*

<sup>225</sup> Sasa hebu tuchukue ninii . . . na ninii . . . uso Wake:

*. . . na upanga mkali, wenyewe makali kuwili, unatoka kinywani mwake: na uso wake ulikuwa kama jua liking’aa kwa nguvu zake.*

<sup>226</sup> Kama mkifungua kwenye . . . hebu tuone, Mathayo 17. Hebu na tulipate tu papa hapa wakati tukiwa kwenye hilo; kwa hiyo tunalipita tu, na wengi wa hao watu wanaolichukua, hebu . . . ama kuliandika, tutawaacha tu walosome kusudi tupate kujuua.

<sup>227</sup> Mathayo 17, vema:

*. . . baada ya siku sita, Yesu amtwa Petro, na Yakobo, na Yohana . . . katika mlima mrefu faraghani,*

*Akageuka sura yake mbele yao: uso wake ukang’aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru.*

<sup>228</sup> Yeye aligeuzwa. Alifanya nini? Akajipitisha Mwenyewe katika kugeuzwa mpaka akaingia katika ile siku ya kuja Kwake. Sasa angalieni, saa chache tu kabla ya haya, Yesu alikuwa ametoa nukuu hii hapa nyuma katika mlango unaofuata, “Amin, nawaambia, ya kwamba wengine wanasimama hapa . . .” Ni wangapi wanajua yale ninayotaka kusema? “Wengine wanaosimama hapa hawatapita, hawatakuwa, mpaka watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Utukufu.” Hiyo ni kweli? Ndipo akawachukua Petro, Yakobo, na Yohana, wale mashahidi watatu, maana katika Agano la Kale kila kitu, kila neno dogo, lilihakikishwa mbele ya mashahidi watatu, na kuwapeleka juu ya mlima.

<sup>229</sup> Angalieni ni kitu gani kilichokuja kwanza. Loo, kamwe siwezi kusimama papa hapa, sina budi kufikia hili. Angalieni! Kitu cha kwanza walichoona ni nini? Walimpeleka Yesu mlimi . . . ama Yeye aliwapandisha, naye akageuka sura mbele yao, akageuka. Vazi Lake likang’aa kama jua katikati ya nguvu zake, ndipo wakamtokea Musa na Eliya. Mwana wa Adamu

anakuja katika umbo gani sasa? Na kwanza, kutokea, watakuwa Musa na Eliya.

<sup>230</sup> Sasa, angalieni, kabla ya kurudi kwa Yesu duniani . . . Sasa, hili kidogo liko mbele ya wakati, bali Roho wa Eliya atarudi duniani na kuigeuza mioyo ya watoto imrudie baba. Biblia ilisema hivyo. Yesu alimwona hapa, mitume walimwona hapa, utaratibu wa kuja kwa Mwana wa Adamu aliyetukuka. Yeye atatukuzwa kisha arudi. Jambo la kwanza, kabla hawajamwona, ilikuwa nini? Eliya. Halafu kitu gani? Musa; Israeli wakirudi kule, washika-sheria. Na kisha Mwana wa Adamu aliyetukuka. Haleluya! Je, mnaona utaratibu wa kuja Kwake? Roho ya Eliya, ama ushuhuda wa wakati wa mwisho wa kanisa. Mnaona, akija katika nguvu apate kumdhahirisha.

<sup>231</sup> Ndipo wale Wayahudi mia moja na arobaini na nne elfu watakusanyika juu ya Mlima Sinai, ambapo Israeli imekuwa ni taifa yenye; taifa la kale kuliko yote ulimwenguni, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni; wana taifa lao wenye; bendera yao wenye; jeshi lao wenye; pesa zao wenye; na kila kitu kingine. Hao ni mmoja wa wanachama wa shirikisho la mataifa kwa sababu wao ni taifa. Yesu alisema hawapaswi kutupwa mpaka mambo yote yatimie.

<sup>232</sup> Siri ya vile kundi hilo la Wayahudi, walioteswa kila mahali, na kufukuzwa, na kufukuzwa na kutupwa nje, kama vile Kanisa kote katika nyakati hizi za kukataliwa, na hata hivyo Yesu alisema, “Mtakapoona mtini ukichipusha majani yake, taifa hilo likirudi lipate kuwa taifa tena, wakati umekaribia, hata mlangoni. Amin nawaambia, Kizazi hiki hakitapita mpaka mambo haya yote yatakapotimia.” Ukoo huu . . . Watu hawa hawatapita. Hitler alijaribu kuwaua, Mussolini alijaribu kuwaua, Stalin alijaribu kuwaua, wengine wote, bali kamwe hawatatiwa dosari, wala kufukuzwa kutoka ardhini, watakuwa ni watu na taifa linalosimama kule. Amina!

<sup>233</sup> Watakuja Musa na Eliya. Loo! Natumaini mnalipata.

<sup>234</sup> Vema, “Jua liking’aa katika nguvu zake,” sura Yake, ikageuka, ikabadilika. Sasa jambo lingine, katika Ufunuo 21:23, ikiwa unataka kuliandika. Katika Yerusalemu Mpya, 21:23, Yeye ni Mwana-Kondoo aliye kwenye Mji, ambaye ni Nuru yake, ikiangaza; kwa maana hawakuhitaji nuru Mjini, jua halitachomoza ndani yake, kwa sababu Mwana-Kondoo aliye katikati ya Mji atakuwa Nuru yake. Nayo mataifa ambao wameokoka watatembea katika Nuru hiyo ya Mwana-Kondoo! Amina! Yeye ndiye Nuru ya Mwana-Kondoo. Loo, hivi hamna furaha juu ya hilo?

<sup>235</sup> Si hilo tu, bali Yeye pia, katika kule kuja (Yohana alimwona katika siku ya Bwana), Jua la haki. Hebu twende kwa Malaki. Malaki, yule nabii wa mwisho wa Agano la Kale. Malaki, mlango wa 4.

<sup>236</sup> Nina hadithi ndogo ya kusimulia kuhusu mke wangu wa thamani anayeketi pale nyuma. Nilimpa wakati mgumu kabla hatujafunga ndoa, nimejaribu kuirekebisha tangu tulipooana. Wala mimi sikujuu kama nilitaka kuoa tena ama la, na kwa hiyo akahuzunika sana. Nami nilifikiri alikuwa ni msichana mzuri sana kumwacha tu aende, niache mtu mwingine amwoe ambaye angemtunza. Nami nikawazia hata sikustahili jambo hilo; wala sistahili, kwa wema wake, kwa vyovoyote vile. Kwa hiyo alikuwa amehuzunika sana wala hakujua la kufanya. Hii imekuwa ni miaka kadhaa iliyopita, yapata miaka ishirini iliyopita. Alihuzunika sana, akaanza kulia mchana na usiku. Nami nilikuwa nikijaribu kumwacha, si kwa sababu sikumpenda, ni kwa sababu sikutaka kuchukua muda wake; maana, nimwache apate mtu fulani, mtu fulani mzuri, maana yeze ni msichana mzuri sana kumwachilia tu aende namna hiyo, na mimi kuchukua...kuambatana tu naye na mambo kama hayo. Na mimi—mimi nilifikiri alinipenda, nami nilijua nilimpenda. Kwa hiyo basi nikawazia, “Vema, nitajaribu tu...Nitafanya miadi na msichana mwingine na kutoka nje, na kumfanya anikasirikie.” Hilo karibu limuue, nilichukia jambo hilo sana baadaye; yeze alihuzunika kabisa. Nikamwambia, nikasema, “Wewe ni msichana mzuri sana, si—sitaki kuchukua muda wako namna hiyo.”

<sup>237</sup> Naye akasema, “Lakini na—nakupenda tu *wewe*, Bill, na huyo ndiye pekee ninayeweza kumpenda.” Kasema, “Ni—nimekupenda sikuzote.”

Nikasema, “Na—nathamini hilo. Lakini,” nikasema, “unajua,” nikasema, “Mimi ni walii mpweke.” Nikasema, “Ni—nitaishi tu kama walii mpweke. Unaona, si—sitaoa kamwe.”

<sup>238</sup> Naye alikuwa amelishikilia sana, mwajua, maskini jamaa huyo. Ndipo akatoka kwenye—kwenye kibanda. Naye akatoka huko nje, kisha akapiga magoti yake, na kusema, “Bwana, sijui la kufanya. Si—sitaki kukosa kukutii, na hata hivyo ninampenda Bill, wala sijui la kufanya. Bwana, waweza kunipa faraja kidogo? Waweza kunisaidia kidogo? Kamwe sikukuomba jambo hili hapo awali maishani mwangu, Bwana, nami natumaini haitanibidi kukuomba tena,” akasema, “bali ikiwa Wewe utanisaidia tu, na uniruhusu kuifungua Biblia hii, Nawe unipe Andiko. Nimewasikia watu wakisema Wewe hufanya hivyo.” Basi alipoifungua, ilikuwa ni Malaki 4:

*Tazama, ninakupa...ama nitawapelekea Eliya nabii  
kabla haijaja siku ile—ile ya kuogofya ya BWANA:*

<sup>239</sup> Akasema, “Niliamka kutoka hapo nikiwa nimeridhika kabisa ya kwamba tutafunga ndoa kwa vyovoyote vile.” Mnaona?

*Kwa maana, tazama, siku inakuja, ambayo itawaka  
kama tanuri; na wote wenye kiburi, naam,...wote  
watendao maovu watakuwa mabua: na siku inakuja*

*ambayo itawateketeza, asema BWANA wa majeshi, nayo haitawaachia mzizi wala tawi.*

*Lakini kwenu mnaolicha jina langu, Jua (J-u-a) Jua la haki litawazukia lenye kuponya katika mbawa zake, . . .*

<sup>240</sup> “Jua likiwaka katika nguvu zake.” Loo! Nguvu za Mwana wa Mungu zikiangaza mionganoni mwetu usiku wa leo. Amesimama katikati ya vinara saba vya taa vya dhahabu katika sifa Zake zenye sehemu saba hapa kama hakimu. Kama Mtu ambaye ameteseka na kutufia sisi, na kuichukua hukumu ya Kiungu juu ya nafsi Yake, naye amekanyaga shinikizo, ghadhabu ya hasira ya Mungu. Kwa mwenye dhambi Yeye ni maporomoko ya kutisha, kwako wewe nafsi iliycoachiliwa juu ya bahari ya maisha. Na kwa Kanisa, Mwokozi mwema, aliyetiwa nanga katika raha, na kusikia kijito cha mawimbi-wimbi wakati umelala na kupumzika kikamilifu ukiwa umeridhika kikamilifu katika Kristo. Ni wakati wa jinsi gani! Akituangazia kwa miale Yake yenye joto, “Msiogope, Mimi Ndimi aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuwa. Mimi ni Mwenyezi, zaidi ya Mimi hakuna mwingine. Mimi ni Alfa na Omega pia, nami nitampa yeye aonaye kiu chemchemi ya maji ya Uzima bure.” Loo, ni ahadi ya jinsi gani na ni suala la upendo wa jinsi gani! Naye Mwana-Kondoo katikati ya ule Mji usiohitaji taa, na Yeye ndiye Jua la haki lenye uponyaji katika mbawa Zake.

Yeye ni Nyinyoro ya Bondeni, Nyota Angavu ya Asubuhi,

Yeye ni mwema kuliko elfu kumi kwa nafsi yangu.

Katika huzuni Ndiye faraja yangu, katika shida Ndiye ngome yangu,

Huniambia nimpelekee haraka kila sumbuko.  
Haleluya!

Yeye ni Nyinyoro ya Mabondeni, Nyota Angavu ya Asubuhi,

Yeye ni mwema kuliko elfu kumi kwa nafsi yangu.

<sup>241</sup> Naam, bwana! Loo, huyo Nyota ya Asubuhi aliye mkuu ametokeza apate kuangaza, akiikaribisha siku inayokuja, akiivurumisha, akisema, “Siku imekaribia kupambazuka, Mwana anakaribia,” Naye anajitokeza nyuma ya nyota zingine zote (Loo, jamani.) mwenye uponyaji katika mbawa Zake.

<sup>242</sup> Sasa turudi kwenye ujumbe wetu. Nasi tunafunga sasa, tupate kujiandaa kwa ajili ya usiku wa kesho, kwa sababu wakati ni saa tatu kasorobo, hatutaki kumchelewesha mtu yeoyote kupita kiasi, kusudi tu tuweze kuwa hapa.

<sup>243</sup> Vema, Jua la haki likiwa na uponyaji katika mbawa Zake. Sasa uso Wake. Yeye alikuwa ni hakimu, ama jambo lingine la kuonyesha ya kwamba alikuwa kwenye siku ya

Bwana. Mnaamini hilo? Yeye alivuka akaingia kwenye siku ya Bwana na kumwona Bwana kama hakimu; sio kama kuhani, sio kama mfalme, bali kama hakimu. Yeye ni Hakimu. Hivi hamwamini hilo? Biblia inasema Yeye ni Hakimu. Naye huyu hapa alikuwa amevaa kabisa kama Hakimu, akionyesha yale aliyokuwa amefanya; kile alichokuwa: kile alichokuwa kwa mwenye dhambi, kile alichokuwa kwa Mkristo. Naye huyu hapa sasa amesimama akiwa na sauti ya maji mengi, nao uso Wake ulikuwa kama jua likiangaza katika nguvu zake.

<sup>244</sup> Sasa matokeo yake, kifungu cha 16. “Na . . .” La, samahani, ni kifungu cha 17:

*Nami nilipomwona, nilianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa . . .*

<sup>245</sup> Jamani! Nabii huyo asingeweza kusimama tena, kuona ono kama hilo. Alininii tu—Nguvu zake zilimtoka, naye akaanguka moja kwa moja chini miguuni Pake kama mtu aliyekufa. Sasa angalieni:

*. . . Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akiniambia, Usiogope. Mimi ni wa kwanza na wa mwisho:*

<sup>246</sup> Loo, jamani! Sio nabii, Mungu! “Mimi ni wa kwanza na wa mwisho. Mimi ndimi mwanzo wa Ufunuo, mwisho wa Ufunuo. Mimi ni Yule aliyekuwako, Mimi ni Yule aliyeko, Mimi ni Yule atakayekuja.” Hebu tuone:

*Mimi ni . . . Mimi . . .*

*. . . Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akiniambia, Usiogope; Mimi ni wa kwanza na wa mwisho:*

*mimi ni yule aliye hai, nami nilikuwa nimekuwa; na, tazama, ni hai milele na milele, (Hivi sasa. Halafu akapiga makelele:) Amina; na nina funguo za kuzimu na . . . mauti.*

<sup>247</sup> Sasa, msiogope. Kwa nini tuogope? Kwa nini Kanisa lishindwe kutimiza ninii Yake . . . kuliwazia Neno Lake? Hebu tusimame hapa kwa dakika moja, maana tunafunga. Kwa nini Kanisa hili liogope kamwe? Ni kitu gani amepata kuahidi ambacho Yeye hajakidhihirisha mbele zetu? Kwa nini uogope hukumu ama mambo yajayo? “Usiogope! Mimi ni Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, na atakayekuja. Mimi ni wa kwanza na wa mwisho. Nina funguo za kuzimu na mauti papa hapa.” Kwa nini? “Nimeshinda na kushinda kuzimu na mauti (Hiyo ni kaburi na jehanamu pia; mauti yenyewe, kuzimu yenyewe.) kwa ajili yenu. Nimeyashinda yote. Ninashinda kuzimu, mauti, kaburi.” Alipokuwa duniani, alikuwa ndiye pekee aliye mku- . . .

<sup>248</sup> Watu wengi wametoka wakaenda wapate kushinda. Mlijua hilo? Napoleon aliondoka akaenda kuupiga ulimwengu, naye

akaushinda kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu. Kwenye umri wa miaka kumi na saba hadi ishirini na mitano, Napoleon alikuwa mpinga pombe, hakuamini katika kunywa pombe au chochote. Akaenda Ufaransa. Yeye hakuwa Mfaransa, alikuwa ametoka kwenye kisiwa fulani, alienda kule akajilipizie kisasi dhidi ya Ufaransa kwa maana hakuipenda, hakupenda Ufaransa. Lakini alishindwa. Naye akaenda kule na kuishinda Ufaransa, kisha akawachukua hao Wafaransa na kuushinda ulimwengu. Ndipo kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu aliketi chini akalia kwa kuwa hapakuwapo na mtu mwingine wa kushinda, basi akafa mlevi sugu. Alishindwa, hata asingeweza kujishinda mwenyewe. Mnaona? Ndipo akakutana na kikomo chake huko Waterloo, alikutana na mwisho wake huko Waterloo. Nimekuwa huko na kuona zile ishara za kale za kumbukumbu na kadhalika huko, tulipokuwa humo nchini. Sasa, hebu tumchukue huyo mshindi, ye ye alianza kama kijana mwanamume naye akachukua upande mbaya wa kushinda, ndipo akafa, kwa aibu.

<sup>249</sup> Lakini kulikuwako na kijana Mwanamume mwingine aliyekuwa ulimwenguni wakati mmoja. Alikufa kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu Naye akashinda kila kitu kilichowea kushindwa. Wakati alipokuwa duniani Yeye alishinda hamaki, kiburi, alishinda maradhi, alishinda ibilisi. Alipokufa, alishinda mauti. Alipofufuka, alishinda kuzimu. Alipaa juu na kushinda kila kitu kilichokuwa dhidi ya binadamu, kikaingia katika shinikizo la mvinyo ya Mungu na kuivunja-vunja na kuyashinda mauti, kuzimu, kaburi, maradhi, kanuni, kila kitu kingine, na kuyashinda yote, kisha akafufuka siku ya tatu na kushinda mazingira yote juu, na kuondoa ukungu huo kati ya Mungu na mwanadamu, na kuunganisha Mbingu na dunia. Utukufu! Loo, jamani! Whiu!

<sup>250</sup> Huyo hapo amesimama yule Mshindi Mkuu tangu alipoipasua pazia vipande viwili, Huyo hapo. Yeye ana funguo za mauti na kuzimu pia zikining'inia ubavuni Mwangu, "Msiogope." Akaweka mkono Wake wa kuume (Nguvu zake) juu yake, na kumwinua kwa nguvu za mkono Wake wa kuume, kasema, "Usiogope, Mimi Ndimi aliyekuwako, na Yeye aliyeko, na atakayekuja. Mimi ni wa kwanza na wa mwisho. Mimi Ndimi niliyekuwa hai, kisha nikafa, na ni hai tena milele. Amina!" Loo!

Lo! Mtazame mshindi mkuu,  
Lo! Mtazame Yeye akionekana dhahiri,  
Huyo hapo amesimama, mshindi mkuu,  
Tangu alipoipasua pazia vipande viwili.

<sup>251</sup> Amina! Akakatilia mbali kila kizuizi kutoka kwa wanadamu, wapate kuunganishwa kama katika bustani ya Edeni. Sasa, mwanadamu... Nilikuwa nikitaka kuliacha, bali nitalisema. Mwanadamu yuna nguvu zote. Hamuamini hilo, bali

ndivyo alivyo. Mwanadamu aliyejitolea kabisa kwa Mungu yuna nguvu zote. Hivi Yeye hakusema, katika Marko 11:22, "Chochote utakachosema, wala usiwe na shaka moyoni mwako, kitatimia. Uliyosema yatakuwa yako"?

<sup>252</sup> Inakuwaje wakati watu wawili walio na nguvu zote wakikutana? Mungu na mwanadamu wanapokuja pamoja, wawili wenye nguvu zote, kitu fulani hakina budi kutikisika. Ninii fulani... Lolute ambalo ungesema kwa nguvu hizo za uumbaji za Mungu mweza yote, ukijua ya kwamba Yeye aliliahidhi, Naye akasema katika Neno Lake, linaumba nguvu zinazoenda huko ng'ambo na kuyatimiza mambo, mambo yasiyokuwako, zinayafanya, kana kwamba yapo, kwa sababu wawili wanaoweza yote wamekutana. Huyo hapo amesimama! Loo, hivi si Yeye ni wa jabu!

<sup>253</sup> Hebu tuone kama tuna mambo mengine mazuri. Kifungu cha 18, sasa kifungu cha 19. Yohana; ni kitu gani kilichotendeka wakati alipouona uso Wake? Matokeo yake? Alianguka miguni Pake; asingeweza kusimama tena, uhai wake wa kibinadamu ulikwisha, asingeweza kufanya hivyo. Yeye alikuwa ni mshindi, alikuwa ameshinda tayari.

<sup>254</sup> Sasa Yeye anatoa amri, ndipo tunaanza kuumaliza mlango huu, kifungu hiki cha 19:

*Basi, uyaandike mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na yale yatakayokuwa baada ya hayo.*

<sup>255</sup> Tulichukua kifungu cha 20:

*Siri ya zile nyota saba ulizoziona katika mkono wangu wa kuume,... ni vile vinara saba vy a dhahabu. Zile nyota saba ni malaika wa yale makanisa saba: na vile vinara saba ulivyoona ni makanisa saba.*

<sup>256</sup> Loo! Linashangaza sana, ewe rafiki. Mwangalie amesimama pale katika ukuu... ukuu wa Uungu Wake. Yeye ni Hakimu, Kuhani, Mfalme, Tai, Mwana-Kondoo, Simba, Alfa, Omega, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. Anakanya shinikizo la ghadhabu ya hasira ya Mungu, na kufurahisha kila kitu, mpaka Mungu akasema msalabani... Wakati alipofufuka, Yeye alisema, "Imekwisha!" Akamfurahisha Mungu sana, hata Roho aliyemwacha akarudi asubuhi ya Pasaka na kumchukua na kumfufua tena kwa ajili ya kutuhesabia haki.

<sup>257</sup> Hapo Yohana aliangalia juu na kumwona amesimama pale akiwa na miguu ya shaba, macho kama miali ya moto ikienda huku na huko kote duniani. Danieli alimwona miaka mia saba kabla ya hapo, mahali papo hapo, namna ile ile, mtu yule yule amesimama pale, Mzee wa siku, na mmoja mfano wa Mwana wa Adamu aliyeungana Naye, na hukumu yote akapewa Yeye, amesimama kwenye Kiti cha Enzi cha Hukumu.

<sup>258</sup> Tukiyaona mambo haya, tunapaswa kuwa watu wa aina gani, enyi marafiki? Mungu awabariki ndilo ombi langu. Mnaona? Mnampenda? Mnamwamini? Je, umeitia nanga nafsi yako ndani Yake?

<sup>259</sup> Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

<sup>260</sup> Kwa utulivu tu na poleple, tunapoenda kuimba polepole, *Nimetia Nanga Nafsi Yangu Katika Mahali Pa Raha*, “Kamwe sitasikia maporomoko ya mawimbiwimbi kuipeleka nafsi yangu mbali, bali itanena amani tamu kwa nafsi yangu.” Kwa utulivu sasa, kwa kicho, kila mtu.

Nimetia nanga nafsi yangu katika mahali pa  
raha,  
Sitaabiri bahari yenze tufani tena;  
Tufani inaweza kuvuma juu ya kilindi cha  
bahari yenze dhoruba,  
Katika Yesu mimi ni salama milele.

Nimetia nanga nafsi yangu katika mahali pa  
raha,  
Sitaabiri bahari yenze tufani tena;  
Tufani inaweza kuvuma juu ya kilindi cha  
bahari yenze dhoruba,  
Katika Yesu mimi ni salama milele.

Niangazie, (Jalia miale ya Utukufu, Bwana,)  
Bwana, iniangazie,  
Jalia Nuru kutoka mnara wa taa iniangazie;  
Loo, niangazie, Bwana, niangazie, (Hebu na  
tumwinilie mikono yetu.)  
Jalia Nuru kutoka mnara wa taa iniangazie.

Kuwa kama Yesu, (Naam, Bwana.) kuwa kama  
Yesu,  
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani  
mpaka Utukufuni,  
Naomba tu kuwa kama Yeye.

[Ndugu Branham anaaaza kuvumisha hiyo pambio—Mh.]

. . . Ee Mwokozi wa ajabu,  
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani  
mpaka Utukufuni,

<sup>261</sup> Ungetaka Uzima Wake uishi ndani yako, ukiakisi Uwepo Wake? Kama ungetaka, nawe hujaupata bado, unaweza kusimama kwa ajili ya maombi? wale ambao wangetaka kukumbukwa katika maombi. Mungu awabariki.

Kutoka hori la Bethlehem... (Endeleeni  
kusimama sasa, bakini tu kwenye...) . . .

alitokea Mgeni, (Utakuwa mgeni kwa ulimwengu.)

Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
Kote katika safari ya maisha, kutoka duniani  
hadi Utukufuni,  
Naomba tu kuwa kama Yeye.

Kuwa tu kama Yesu, kuwa tu kama Ye-...  
(Hiyo ndiyo shauku yangu.)

Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
Kote katika safari ya maisha, kutoka duniani  
hadi Utukufuni,  
Naomba tu kuwa kama Yeye.

[Ndugu Branham anaanza kuivumisha pambio—Mh.]  
...mpole, mnyenyeketu na mpole.

<sup>262</sup> Sasa, Baba wa Mbinguni, watu wengi wamesimama kwa miguu yao ambaao wanataka kukupokea. Wemechoshwa na huku kuyumbishwa huku na huku, bila kujua wanakoenda, kutoka kwenye masumbuko ya maisha; na wakijua labda kabla ya mapambazuko moyo utaacha kudunda, ndipo lile poromoko kuu, maporomoko, mbele yao, nafsi inayoelea. Wamekuwa kama wao wenyewe, wamekuwa kama ulimwengu, bali wanataka kuwa kama Wewe sasa, Bwana. Wapokee katika Ufalme Wako, wao ni Wako, Baba, kwa sababu Wewe unaijua mioyo yao na makusudi ya mioyo yao. Nawe umeliandika, na kusema kwa midomo Yako mwenyewe, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na atamwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Pia ulisema, Bwana, “Heri ye ye asomaye na ye ye ayasikiaye maneno ya unabii wa Kitabu hiki, kwa kuwa wakati u karibu.” Wanatambua ya kwamba wakati umekaribia. Hawawezi kuelea tena, Bwana. Shusha kamba okozi, wavute Kwako, Bwana. Jalia waende tangu usiku wa leo, wakiiakisi Nuru ya Yesu Kristo. Ninawakabidhi Kwako, Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia wamfuate Bwana kwa unyenyekevu katika ubatizo hapa kanisani; mweke Roho Mtakatifu maishani mwao ili kwamba waweze kuwa kama Yesu siku zao zilizosalia. Tunaomba katika Jina Lake.

Kuwa tu kama Yesu, kuwa kama . . .

<sup>263</sup> Baadhi yenu nyote mnaosimama karibu ama mnaoketi karibu na watu hao, ambaao ni Wakristo, nyosheni mikono yenu mshike mkono wao na muwape mikono. Wekeeni mkono wenu juu yao, “Mungu asifiwe kwa ajili ya nafsi yako.” Madhababu yetu yote yamejazwa na watoto na kadhalika, hatuwezi kuwapandisha hapa juu.

Kupitia kwa safari ya maisha, kutoka duniani  
hadi Utukufuni,  
Naomba tu kuwa kama Yeye.

Niangazie, Loo, niangazie,  
 Jalia Nuru kutoka kwenye mnara wa taa,  
     iniangazie;  
 Loo, niangazie, Bwana, niangazie,  
 Jalia Nuru kutoka kwenye mnara wa taa,  
     iniangazie.

<sup>264</sup> Mnajisikia vizuri sana? Hivi hamjisikii vizuri? Hivi huna furaha kwamba wewe ni Mkristo? Peana mikono na mtu fulani anayeketi karibu na wewe sasa, wakati tunapoenda kuimba wimbo, *Tutatembea Nuruni*, Nuru hii nzuri, Nuru ya Bwana Yesu Kristo akidhihirishwa katika mwili.

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri sana,  
 Njoo ambapo umande wa rehema unang'aa;  
 Tuangazie kote, mchana na usiku,  
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Uimbeni, kila mtu:

Tutatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri,  
 Njoo mahali ambapo umande wa rehema  
     unang'ara;  
 Tumulikie kote, mchana na usiku,  
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.  
 Njoni, enyi watakatifu wote wa Nuru  
     mkatangaze,  
 Yesu, Nuru ya ulimwengu;  
 Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,  
 Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Inua mkono wako sasa:

Tutatembea katika Nuru hii, Nuru nzuri,  
 Njoo ambapo umande wa rehema unang'aa;  
 Tuangazie kote, mchana na usiku,  
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutaendelea kutembea katika Nuru hii, ni  
     Nuru nzuri sana,  
 Huja mahali ambapo matone ya umande wa  
     rehema unang'ara sana;  
 Tuangazie tu kote, usiku na mchana,  
 Yesu, Yeye ni Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea katika Nuru hii (Nuru ya Injili),  
     Nuru nzuri,  
 Huja ambapo matone ya umande wa rehema  
     yanang'aa;  
 Tuangazie kote, mchana na usiku,  
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

<sup>265</sup> Huko nyuma mwanzoni, huko Pentekoste wakati Roho Mtakatifu aliposhuka juu ya Kanisa. Ujumbe ulishuka ukaja Smirna; hapo alisimama Ireneo, yule mtakatifu mkuu wa

Mungu, akinena kwa lugha, nguvu za Mungu, kufufua wafu, kuwaponya wagonjwa, Yeye alikuwa akitembea katika Nuru. Baada yake akaja Columba, yule mtakatifu hodari wa Mungu. Watakatifu wengine wengi mashuhuri, wakiubeba Ujumbe, wakitembea katika Nuru, Nuru ya Injili, Nuru ile ile iliyoangaza kwenye Siku ya Pentekoste; Kristo akisimama katikati ya watu Wake, na hivyo vinara saba vya taa vikiakisi nuru Yake kama jua katikati ya joto lake.

<sup>266</sup> Sisi hapa katika mwaka wa 1961:

Tunatembea katika Nuru hii, ni Nuru nzuri  
sana,  
Inakuja mahali ambapo umande wa rehema  
unang'aa;  
Loo, tuangazie kote, usiku na mchana,  
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Na tusimame:

Tutaendelea kutembea katika Nuru hii, ni  
Nuru nzuri sana,  
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema  
yanang'aa;  
Tuangazie kote mchana na usiku,  
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Mnampenda?

Nampenda, nampenda,  
Kwani (kwa sababu tu) alinipenda kwanza,  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>267</sup> Kamwe sitarudi tena kwenye mambo ya ulimwengu. Mimi nimekuwa kwa ulimwengu na ulimwengu umekufa kwangu. Mimi hutembea tu ndani ya Kristo, nikiongozwa na Roho Mtakatifu. Ninampenda kwani Yeye ananipenda, Naye huniangazia baraka Zake, akinipa mkono wa kuume wa ushirika katika Ufalme Wake. Sasa sisi ni wana na binti za Mungu, na haijadhihirika bado tutakavyokuwa mwishoni; bali tunajua ya kwamba tutakuwa na mwili kama Wake uliotukuzwa, kwa kuwa tutamwona kama alivyo.

Basi tutatembea katika Nuru, ni Nuru nzuri,  
Inayokuja mahali ambapo umande wa rehema  
unang'ara;  
Tuangazie kote mchana na usiku,  
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

<sup>268</sup> Je, mnampenda? Mnajua, baada ya ujumbe unaokata-kata na kadhalika, ninapenda kuwasikia watu wakiingia katika nyimbo na kuanza kuabudu na kuimba katika Roho. Hakuna kitu kilicho kizuri kuliko kuimba kuzuri kwa kale. Hiyo ni kweli. Ninapenda kuimba kuzuri kwa kipentekoste kwa

mtindo wa kale; sio hizo sauti zilizofunzwa kupita kiasi zinazoshikiliwa mpaka zinakoroma nao uso unakuwa bluu, wala hawajui wanachoimba. Ninapenda mtu ambaye labda asingeweza kuibeba tuni kwenye kikapu lakini ana Baraka za Kipentekoste, anazoimbia sasa. Loo, jinsi—jinsi zilivyo tukufu hizo sauti tamu za msalabani! Loo, jamani!

Wimbo wetu wa kupumukana sasa:

Peleka Jina la Yesu,  
Mtoto wa huzuni na majonzi;  
Litakupa furaha na faraja,  
Peleka uendako.

Kesho usiku saa moja, saa moja kamili, ibada itaanza.

Tukiliinamia Jina la Yesu,  
Tukisujudu miguuni Pake,  
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,  
Safari yetu itakapokamilika.

Hebu tuimbe sote sasa:

Peleka Jina la Yesu,  
Mtoto wa huzuni na majonzi;  
Litakupa furaha na faraja,  
Loo, peleka uendako.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu! (Ni tamu!)

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

<sup>269</sup> Sasa, tuliumaliza usiku wa leo. Ninii...ndio kwanza waniulize sasa, "Kama kutakuwako na ibada asubuhi?" La, sio kesho, pumzikeni vizuri kesho. Labda kesho usiku, sitaweza kuumalizia ujumbe huo, kwa hiyo nitauchukua kesho yake. Wakati wowote nikishindwa kwenye...ujumbe huu kamili, nitaubeba kesho yake. Lakini tumeyamaliza haya, ninaamini mko tayari kwa ajili ya Nyakati za Kanisa. Sivyo? Vema.

Na tuinamishe vichwa vyetu tunapoimba kwa utulivu sasa:

Tukiliinamia Jina la Yesu, (Kila ulimi utalikiri.)  
Tukisujudu miguuni Pake,  
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,  
Safari yetu itakapokamilika  
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! (Jinsi lilivyo tamu!)  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.



*ONO LA PATIMO* SWA60-1204E

(The Patmos Vision)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 4 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwénye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)